SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

## Mkandarasi 'aingia mitini' utekelezaji mradi wa milioni 194/-



UKURASA 5







Nipashe
Jumapili Novemba 28, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
JUMAPILI
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0580778
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Migogoro ya ndoa ilivyo tishio nchini

**Ni** sehemu ya mzizi wa majambazi, mauaji...*Endelea ukurasa 3*



Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na mgeni wake, Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya ziara ya Kitaifa ya siku tatu hapa nchini. **PICHA: IKULU**

## Rais Samia, Museveni kuinua uchumi, ajira

UKURASA 2

UKURASA WA 4

### WANAWAKE WALIA KUNYIMWA NAFASI NYETI VYAMA VYA SIASA

VIONGOZI wanawake kutoka vyama 19 vya siasa nchini, wamedai mfumo...

UKURASA WA 4

### LHRC: UKATILI KIJINSIA BADO TATIZO NCHINI

IDADI ya matukio ya ukatili wa kijinsia imeongezeka nchini, ikibainishwa kuwa yanayoripotiwa mtandaoni...

UKURASA WA 4

### WAIPONGEZA SERIKALI KWA KUWAKUMBUKA

BARAZA la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NACONGO) limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan...

## Mikoa vinara chanjo corona yatajwa, imo inayosuasua

UKURASA 2

MICHEZO NI SIMBA VS RED ARROWS UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Taratibu bomba la mafuta zakamilika

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema karibu kazi zote muhimu za kukaribia kuanza utekelezaji wa mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima mpaka Tanga zimekamilika ikiwamo mikataba na kandarasi za awali.

January alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam katika kongamano la mafuta na gesi lililoandaliwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Uganda (PSFU) kujadili mradi huo ambao umefikia hatua nzuri ya utekelezaji.

"Kazi za ujenzi mdogo zimeanza, tutakuwa na kambi kubwa pale Nzega mkoani Tabora, kiwanja kimepatikana na wenyewe wameanza kusafisha, ajira zitatoka nyingi," alisema.

January alikumbusha kuwa asilimia 80 ya mradi huo ipo Tanzania na una manufaa kwa wafanyabiashara kujengewa uwezo, lakini kuzijua na kuzifikia fursa ni jambo lingine.

"Taasisi yetu ya sekta binafsi kwa kushirikiana na wenzao wa Uganda wameandaa kongamano la pamoja la mafuta na gesi ili kujadili mradi wenyewe, mahali tulipo, fursa zilizopo, mwelekeo, masuala ya sheria, mazingira, kodi na namna sekta binafsi nchi zote mbili zinazifikia na kunufaika nazo," alisema.

Waziri huyo alisema kongamano hilo ni muhimu kwa kuwa linatoa elimu zaidi kwa Watanzania na sekta binafsi na kwamba mradi huo ni fursa kubwa kuchangia ukuaji wa uchumi na ajira.

Alisema wanaamini fedha zitakazotumika kwa ujenzi huo, ambazo ni zaidi ya dola za marekani bilioni 3.5, kwa sehemu kubwa zinastahili kuingia kwenye mzunguko wa uchumi wa nchi hizo mbili kulingana na kandarasi zitakazotolewa.

Mkurugenzi wa TPSF, Francis Nanai, alisema sekta binafsi zimekutana ili kuzungumza masuala ya mafuta na gesi hususani bomba hilo la mafuta.

Alisema gharama za utengenezaji wa bomba hilo ni zaidi ya dola bilioni 3.5 lakini wakiangalia mnyoyoro mzima wa thamani unazidi dola bilioni 20.

"Tumekutana kuangalia je, Watanzania wana ufahamu wa mradi huu? Kama hawaufahamu ni fursa kupitia kongamano hili kuufahamu, pia tunaangalia namna gani Watanzania watanufaika moja kwa moja au kupitia mambo mengine ya kibiashara, kama kuna matatizo ya kikodi au kisheria tutapata majibu leo (jana)," alisema.

# Rais Samia, Museveni kuinua uchumi, ajira

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, wamekubaliana mambo saba yenye lengo la kuinua uchumi na kutoa ajira kwa wananchi wa nchi hizo mbili.

Miongoni mwa mambo hayo ni matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam kupitisha shehena la vifaa vya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganga hadi Tanga, Tanzania.

Makubaliano hayo yametokana na mazungumzo waliyofanya jana Ikulu jijini Dar es Salaam baada ya Rais Museveni kutua nchini kwa ziara ya siku tatu.

Akizungumza mara baada ya mazungumzo yao, Rais Samia alisema jambo la kwanza walilokubaliana ni kukuza na kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya nchi hizo mbili.

Alisema wamewaelekeza mawaziri wa sekta kukutana mara kwa mara ili kutatua matatizo yanayojitokeza katika maeneo yao na kuhakikisha ushirikiano huo unaendelea kuimarika.

Rais Samia alitaja jambo la pili kuwa ni ushirikiano katika sekta ya uwekezaji kwa kuwa Uganda ni nchi ya pili katika uwekezaji Tanzania katika ukanda wa Afrika Mashariki, ikiwekeza miradi 45 yenye thamani ya dola za Marekani milioni 114 iliyotoa ajira kwa Watanzania 2,150.

Pia alisema zipo kampuni mbalimbali za Tanzania zilizowekeza nchini Uganda.

Jambo la tatu ni ushirikiano wa biashara, Rais Samia akifafanua kuwa kwa kipindi cha miaka saba biashara kati ya nchi hizo imeendelea kukua, ujazo wa biashara umeongezeka kutoka Sh. bilioni 200 mwaka 2014 hadi Sh. bilioni 607 mwaka 2020.

"Kama mnakumbuka tulikuwa na vikwazo kama hivi Kenya na tulipokwenda na kuwataka mawaziri na wataalamu wakae. Sasa biashara kati ya Tanzania na Kenya imekuwa mara sita zaidi, ni matgemeo yetu tukitatua vikwazo na Uganda, biashara itakua zaidi," alisema.

Pia alisema wamezungumzia kuhusu ukuaji wa biashara, matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam ambapo Rais Museven alieleza hiyo ni aibu mpaka leo bandari hiyo imefikia kusafirisha tani 138,262 kwenda Uganda wakati wanatumia nyingine kwa mamilioni ya tani.

Rais Samia alisema jambo lingine walilolizungumza ni utekelezaji wa kimkakati unaohusisha barabara zinazounganisha nchi hizo na nchi za jirani pamoja na miradi ya umeme wanayoifanya kwa pamoja.

Pia alisema wamezungumzia mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi Afrika Mashariki, mradi wa ICO kutoka Hoima Uganda hadi Tanga ambapo Mei mwaka huu nchi hizo zilikamilisha utiaji saini mikataba mbalimbali.

Rais Samia alisema wamekubaliana kushirikiana kuweka kiwanda cha kuzalisha chanjo, zikiwamo za UVIKO-19.

"Chanjo ziwe za UVIKO au chanjo nyingine kwa wanadamu na wanyama, tumewataka wataalamu wetu wakae wajadiliane tutakwenda vipi kwenye kiwanda hiki," alisema.

Pia alisema wamekubaliana mkutano wa kamati ya kudumu ya ushirikiano (JPC) wakutane mwishoni mwa mwezi au mwaka huu kuzungumzia yote yaliyopo kwenye mradi huo.

Rais Museven alisema walikuwa na pendekezo la kukunja vyuma vya bomba la mafuta Tanzania lakini wameona juhudi hizo zinaweza kuchelesha mradi, hivyo wameona kampuni zilizokuwa zimepanga kukunya nje zifanye hivyo.

"Hapa tutakosa ajira Watanzania na Waganda na fedha kiasi lakini acha tuanze, nilipoangalia hesabu ya kujenga bomba hili la mafuta ni dola milioni 1,300.

"Kwa hizo dola milioni 323 ndizo za kununua vyuma vya kutengeneza bomba kuvikunja na kuvipaka rangi. Usafiri kwa bahari ni dola milioni 52. Kizuri wakikunja, kupaka rangi, kusafirisha haziwezi kutumika vizuri bila kuzichoma moto ili vishikane," Rais Museveni alifafanua.

Alisema kiwanda cha kuchoma vyuma hivyo watakijenga Igunga mkoani Tabora na kitagharimu dola milioni 272, usafiri wa ndani dola milioni 43 na kujenga bomba, kuchimba na kuliweka itagharimu dola milioni 684.



Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO), Lilian Badi, akionyesha tuzo ya mchango uliotukuka alioutoa kwa Chuo Kikuu cha Iringa, baada ya kukabidhiwa katika Mahafali ya 24 ya chuo hicho, mjini Iringa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mikoa vinara chanjo ya corona yatajwa

**Na Mary Geofrey**

MSIMAMIZI wa Mpango wa Taifa wa Chanjo, Dk. Florian Tinuga, amesema baadhi ya mikoa inafanya vizuri katika utoaji wa chanjo ya UVIKO-19.

Ameitaja mikoa hiyo kuwa ni Ruvuma, Kagera, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam.

Vilevile, ametangaza orodha ya mikoa inayosuasua kwenye utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 ikiijumuisha Singida, Songwe na Njombe.

Alibainisha hayo alipozungumza katika semina ya waandishi wa habari kwa njia ya mtandao wa zoom kuhusu afua za kinga dhidi ya tishio la wimbi la nne la UVIKO-19 pamoja na chanjo.

Msimamizi huyo alisema kuwa kwa sasa baada ya kubaini mikoa ambayo haifanyi vizuri katika utoaji wa chanjo, wanafanya ufuatiliaji kwa lengo la kubaini vikwazo.

Dk. Tinuga alisema wamebaini vikwazo katika baadhi ya maeneo wananchi wanataka chanjo iwafuate maeneo wanapoishi kama kwenye mikusanyiko na sio wao kuifuata vituoni.

Alisema ili nchi iwe salama, Watanzania wanatakiwa kupata chanjo kwa asilimia 60 hadi 70.

Dk. Tinuga, akielezea hali ya sasa ya usambazaji wa chanjo, alisema Tanzania ina chanjo za aina tatu za UVIKO-19 zinazotolewa zikiwa jumla ya dozi milioni nne ambazo zimepitishwa.

Profesa wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya Muhimbili (MUHAS), Deodatus Kakoko, alitaja sababu ya wananchi wengi kutojitokeza kuchanja ni kutokana na imani potofu, hivyo alishauri kufanyika kwa utafiti dhidi ya imani hizo kwa lengo la kuhamasisha watu kuchanja.

Mwakilishi wa Shirika la AMREF Health Africa, Dk. Ritha Mtayoba, alisema wamekuwa wakishirikiana na serikali kutoa elimu kuhusu UVIKO-19 kupitia miradi yao iliyopo katika mikoa 19 nchini na kuwezesha kuwafikia wananchi wengi. Msemaji Mkuu wa Serikali, Greyson Msigwa, alisema Tanzania ina waandishi wa habari wanaotambulika 978 ambao wako kwenye vyombo mbalimbali vya habari.

Msigwa aliwataka waandishi hao kutumia vyombo vyao kuhamasisha chanjo hiyo kwa kuwaalika wataalamu wa afya kwenye vyombo vyao ili kuwaonyesha Watanzania usalama wa chanjo na kuondoa imani potofu iliyopo dhidi ya chanjo ya UVIKO-19.

## HABARI KITAIFA




Mwenyekiti wa Chama cha Majaji Wanawake Tanzania (TAWJA), Jaji Joacquine De Mello (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa TaMcare, Mchungaji Dk. Enock Mlyuka (kulia), wakizindua Kliniki ya Ndoa na Uhusiano hivi karibuni, Dar es Salaam. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Emmy Hudson. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Migogoro ya ndoa hatari kwa taifa

**Na Mwandishi Wetu**

MIGOGORO ya ndoa ni janga jipya kwa ustawi wa taifa. Hali hiyo inatokana na kushamiri kwa migogoro na kuvunjika kwa ndoa huku athari zake kijamii na kiuchumi zikiwa kubwa.

Hayo yalibainika hivi karibuni mkoani Dar es Salaam katika uzinduzi wa programu maalum kwa ajili ya kuipatia ufumbuzi migogoro ya ndoa ambayo imesababisha athari mbalimbali zikiwamo kusambaratika kwa ndoa, mauaji ya wanandoa kwa sababu ya wivu wa kimapenzi, ongezeko la watoto wa mitaani na wanaolelewa na mzazi mmoja.

Katika uzinduzi wa program hiyo, maarufu kama Kliniki ya Ndoa na Uhusiano, mwishoni mwa wiki iliyopita, wadau mbalimbali walieleza ukubwa wa tatizo tofauti na inavyolichukulia.

Hali halisi inaonyesha kwamba migogoro na kuvunjika kwa ndoa vinashika kasi na hata kutishia nguvu kazi ya taifa kwa kuwa waathirika wa tatizo hilo ni watu ambao ni tegemeo katika kufanya kazi.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Ofisa mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Emmy Husdon, alisema migogoro ya ndoa imesababisha ongezeko la talaka katika taasisi hiyo, hali ambayo inaonyesha tatizo ni kubwa,

"Kwa ujumla, kasi ya usajili wa talaka ni kubwa na hii inaonyesha wazi kwamba migogoro katika ndoa inazidi kushika kasi. Juhudi za ziada zinatakiwa kwa wadau mbalimbali ili kupunguza tatizo hili," alisema Hudson.

Taarifa za utafiti kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), zinaonyesha kuwa talaka nchini zimeongezeka kutoka asilimia 1.1 mwaka 2008/09 hadi asilimia 2.9 mwaka 2017/18 huku taarifa kutoka RITA zikibainisha kuwa kwa mwaka 2020/21 pekee, talaka 551 zilisajiliwa nchini.

Aidha, kwa Mkoa wa Dar es Salaam pekee, kwa mujibu wa Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, katika hotuba yake jijini Dodoma, mashauri ya ndoa na talaka kwa mwaka 2017 hadi 2019 yalikuwa 4,200.

"Inawezekana talaka ni nyingi kuliko takwimu hizi kwa kuwa watu wengi hawajui kusajili matamko ya talaka kutoka mahakamani ili wapate vyeti. Pia wako wanandoa ambao hutengana na kupeana talaka mitaani kienyeji pasipo kufuata taratibu za shEria," alisema Mchungaji Dk. Enock Mlyuka, Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and child Care (TaMCare) Foundation, asasi inayojishugulisha na masuala ya ndoa na malezi ya watoto.

Aliongeza kuwa takwimu hizo zinaonyesha kwamba migogoro na kuvunjika kwa ndoa ni janga la taifa, ndiyo maana taasisi yake imeamua kuanza kutafuta suluhisho la tatizo hilo.

**ATHARI KUBWA**

Kutokana na kushamiri kwa migogoro na kuvunjika kwa ndoa, Dk. Mlyuka anabainisha kwamba kuekuwa na athari kubwa ambazo zinasababisha mmomonyoko wa maadili na kupungua kwa tija na ufanisi kazini.

"Migogoro na kuvunjika kwa ndoa kumesababisha kuongezeka kwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji ndani ya ndoa na matokeo ya wanandoa na wapenzi kuuana. Waathirika wa vitendo hivi ni wanawake na watoto.

"Migogoro ya ndoa pia husababisha matatizo ya kiafya hasa msongo wa mawazo. Athari zake ni kubwa kiroho, kiuchumi, kisaikolojia na kiafya. Pia watoto wanaathirika zaidi katika makuzi yao na kukosa haki ya kuishi na wote wawili hivyo kusababisha mmomonyoko wa maadili," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Majaji Wanawake Tanzania (TAWJA), Jaji Joacquine De Mello, aliyekuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa program hiyo, alisema ndoa ndiyo msingi wa kila kitu hivyo kliniki hiyo itasaidia kulipatia ufumbuzi tatizo hilo ambalo linatishia ustawi wa taifa.

"Tunaishi katika jamii inayobadilika kwa kasi. Kwa vyovyote vile mabadiliko haya hayaziachi ndoa na familia zetu salama. Tumeshuhudia uwapo wa mmomonyoko mkubwa wa maadili, hujuma na manyanyaso baina ya wanafamilia," alisema.

Jaji De Mello alisema familia bora ni jambo muhimu kwa ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla, hivyo kupungua kwa migogoro ya ndoa kutawezesha kupungua kwa maradhi kama vile msongo wa mawazo na jamii kuishi katika amani na furaha.

"Maendeleo ya taifa yanahitaji ndoa imara. Ni ukweli usiopingika kwamba tukiwa na ndoa imara, tutakuwa na familia imara. Tukiwa na familia imara, tutakuwa na jamii imara na tukiwa na jamii imara, tutakuwa na taifa imara kwani ndoa ni msingi wa kila kitu," alisisitiza.


## MEM AUCTIONEERS AND GENERAL BROKERS LTD

**HEAD OFFICE: P.O.BOX 32830 DAR ES SALAAM, BRANCH OFFICE: P.O. BOX 76 HIMO MOSHI**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na kiwanda cha sukari **(TPC LTD);** Tutauza kwa mnada wa hadhara magari, matrekta na vitu mbalimbali kama ilivyooredheshwa hapo chini. Mnada utafanyika tarehe 08/12/2021 kuanzia saa 4.00 asubuhi Kiwandani TPC LTD, Moshi, Kilimanjaro. Mali zitakazouzwa ni kama ifuatavyo;

| LOT NO. | AINA YA MASHINE | TPC NA. | TOLEO | MWAKA WA MATENGENEZO | NAMBA YA USAJILI | USHURU WA FORODHA | PUNGUZO KWA WAAJIRIWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML150 | RANGER | 2016 | T789DLD | PAID | YES |
| 2 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML134 | RANGER | 2015 | T928DFH | PAID | YES |
| 3 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML124 | RANGER | 2014 | T221BDB | PAID | YES |
| 4 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML123 | RANGER | 2014 | T201DBD | PAID | YES |
| 5 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML135 | RANGER | 2015 | T268DGC | PAID | YES |
| 6 | FORD PICK-UP SINGLE CAB | ML117 | RANGER | 2014 | T900CTE | PAID | YES |
| 7 | BELL TRACTOR | MF60 | BELL | 2001 | T667AAT | PAID | YES |
| 8 | BELL TRACTOR | MF61 | BELL | 2001 | T944AAT | PAID | YES |
| 9 | BELL GRADER | MG9 | BELL770D | 2005 | T840ANZ | EXEMPTED | NO |
| 10 | BELL FRONT LOADER | ME6 | LOGGER | 2004 | T696ASQ | EXEMPTED | NO |
| 11 | KOMATSU FRONT END | ME6ME14 | WA380-3A | 2007 | T270ASW | PAID | NO |
| 12 | BACK HOE LOADER | ME18 | LOADER 580M | 2012 | T383CRH | PAID | NO |
| 13 | BELL GRADER | MG11 | 770G | 2011 | T519BSS | PAID | NO |
| 14 | KOMATSU FRONT END | MG15 | WA380-3 | 2009 | T436BLT | EXEMPTED | NO |
| 15 | LORRY NISSAN DIESEL | MR20 | UD | 2010 | T722CAY | PAID | NO |
| 16 | RENAULT TIPPER LORRY | MR15 | VE6 | 2008 | T560BDW | PAID | NO |
| 17 | RENAULT TIPPER LORRY | MR16 | VE6 | 2008 | T541BDW | PAID | NO |
| 18 | LEYLAND ASHOK | MR17 | 912 | 2007 | T152BES | PAID | NO |
| 19 | TOYOTA COASTER | MR89 | 1HZ | 2010 | T936BNP | PAID | NO |
| 20 | NISSAN UD DIESEL BOWSER | MR19 | UD | 2011 | T914BYH | PAID | NO |
| 21 | SLASHER | MP64 | POWA | N/A | N/A | N/A | YES |
| 22 | FERTILIZER APPLICATER | MP60 | REAPER | N/A | N/A | N/A | YES |
| 23 | FERTILIZER APPLICATER | MP49 | REAPER | N/A | N/A | N/A | YES |
| 24 | BOOM SPRAYER | MP74 | BERTHOUD | N/A | N/A | N/A | YES |
| 25 | CONCREATE MIXER | MU69 | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 26 | CONCREATE MIXER | MU68 | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 27 | BOOM SPRAYER | MP105 | BERTHOUD | N/A | N/A | N/A | NO |
| 28 | KUHN SLASHER | MP75 | BPR305 PRO | N/A | N/A | N/A | NO |
| 29 | MUD TRAILLER | MP60 | DEVES | N/A | N/A | N/A | NO |
| 30 | HONDA WATER PUMP | MU2 | HONDA | N/A | N/A | N/A | YES |
| 31 | KUDU ROTARY SLASHER | MU46 | 750 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 32 | KUHN MUTLILONGER SLASHER | MP93 | KUNH | N/A | N/A | N/A | NO |
| 33 | SLASHER | MP45 | SLASHER | N/A | N/A | N/A | NO |
| 34 | LAWN MOWER SLASHER | MP44 | MASTER | N/A | N/A | N/A | YES |
| 35 | GENERATOR | GEN124 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 36 | GENERATOR | MU101 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 37 | GENERATOR | GEN102 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 38 | GENERATOR | GEN81 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 39 | GENERATOR | GEN118 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 40 | GENERATOR | GEN103 | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 41 | KUDU ENGINE | MU80 | HONDA GX390 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 42 | GENERATOR | N/A | HONDA GX270 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 43 | HONDA GENERATOR | N/A | HONDA GX160 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 44 | HONDA WATER PUMP | N/A | HONDA GX160 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 45 | HONDA WATER PUMP | N/A | HONDA GX160 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 46 | HONDA WATER PUMP | N/A | HONDA GX160 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 47 | CHAIN SAW | MU133 | STIHL MA6610 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 48 | CHAIN SAW | MU134 | STIHL MA6610 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 49 | CHAIN SAW | MU132 | STIHL MA6610 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 50 | CHAIN SAW | MU107 | STIHL MS382 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 51 | CHAIN SAW | MU141 | STIHL MS382 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 52 | CHAIN SAW | MU122 | STIHL MS382 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 53 | RAIL GRINDER | MU109 | GEISMAR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 54 | BRUSH CUTTER- | N/A | MARUYAMA | N/A | N/A | N/A | YES |
| 55 | BRUSH CUTTER | MU96 | MARUYAMA | N/A | N/A | N/A | YES |
| 56 | BRUSH CUTTER | MU106 | STIHL FS450 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 57 | LAWN MOWER | MU105 | PROFESSIONAL | N/A | N/A | N/A | YES |
| 58 | LAWN MOWER | MU119 | HONDA196 | N/A | N/A | N/A | YES |
| 59 | MIST BLOWER | MU04 | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 60 | MIST BLOWER | N/A | MARUYAMA MD180DX | N/A | N/A | N/A | YES |
| 61 | MIST BLOWER | N/A | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 62 | MIST BLOWER | N/A | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 63 | MIST BLOWER | N/A | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 64 | MIST BLOWER | N/A | WARRIOR | N/A | N/A | N/A | YES |
| 65 | LOW BED | MT71 | ANGLOCO SPM UK 111A | N/A | N/A | N/A | NO |
| 66 | FERTILIZER APPLICATER | MP6 | SPREADER | N/A | N/A | N/A | YES |
| 67 | PRINTING ACCESSORIES | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 68 | VARIOUS PARTS FOR BOOM SPRAYER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 69 | VARIOUS PARTS FOR KOMATSU FRONT END LOADER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 70 | VARIOUS PARTS FOR KUHN SLASHER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 71 | VARIOUS PARTS FOR CAT& GRADER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 72 | VARIOUS PARTS FOR ISUZU CVR | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 73 | VARIOUS PARTS FOR MITSUBISH CANTER | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 74 | BRONZE &TILES | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 75 | VARIOUS GASKET KITS,RINGS, "O"RINGS & SEALS | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 76 | KEMGUARD&DISPENSERS | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 77 | VARIOUS SIZES OF WINDOW FRAMES | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 78 | VARIOUS SIZES OF WINDOW FRAMES | N/A | | N/A | N/A | N/A | NO |
| 79 | WATER STORAGE TANK 10,000 LTS | N/A | SIM TANK | N/A | N/A | N/A | NO |
| 80 | WATER STORAGE TANK 5,000 LTS | N/A | SIM TANK | N/A | N/A | N/A | NO |

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mali zitauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa fedha taslimu ya 25% mara tu baada ya nyundo ya dalali kutua na salio la 75% kulipwa ndani ya saa 48.
3. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti namba mbili hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mali itauzwa kwa mshindi wa pili.
4. Ukaguzi wa mali utafanyika tarehe 06/12/2021 na 07/12/2021 kuanzia saa Tatu asubuhi mpaka saa kumi jioni.
5. Mnunuzi atatakiwa kuondosha mali katika eneo la mnada mara tu baada ya kukamilisha taratibu za malipo na kodi za serikali.
6. Mali zote zitakazouzwa chini ya milioni moja zitatakiwa kulipiwa kikamilifu siku hiyo hiyo na kuondolewa eneo la mnada.
7. Kwa maelezo zaidi wasiliana na **Dalali kwa Na. 0713/0754 262 400, 0756 606 671**

216581102

# LHRC: Ukatili kijinsia bado tatizo

**Na Christina Mwakangale**

IDADI ya matukio ya ukatili wa kijinsia imeongezeka nchini, ikibainishwa kuwa yanayoripotiwa mtandaoni yameongeka kutoka 249 mwaka 2019 hadi kufikia 1,800 mwaka 2021, huku waathiriwa zaidi wakiwa wanawake na watoto.

Takwimu hizo ni kwa mujibu wa Haki Kiganjani, mfumo ambao hutoa fursa kwa wananchi kutoa taarifa kuhusu matukio hayo kupitia simu za mkononi unaoratibiwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Akiwasilisha takwimu hizo jana kwenye maonyesho ya kidigitali katika siku 16 za kupinga ukatili ya kijinsia jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, alisema wanawake na watoto ni waathirika wakubwa huku baadhi wakiuawa na kubakwa. Pia alibainisha mikoa iliyokithiri matukio zaidi mwaka huu ni Songwe ulioripotiwa kuwa na matukio 207, Mara (206), Morogogo (191) na Katavi 142. Kati yake, baadhi ya matukio yalihusu shambulio, kubakwa, kutoroka, kufukuzwa na mauaji.

"Wanawake na watoto waathirika zaidi. Mwaka 2019 matukio yaliyoripotiwa ni 249, mwaka 2020 yalikuwa 1,407 na mwaka huu 1,800, utaona ongezeko.

"Huu ndiyo umuhimu wa kukua teknolojia, kwamba watetezi wa haki wanaweza kuwasiliana na waathirika kwa hatua zaidi," alisema Anna.

Mkurugenzi huyo alisema kwa kipindi cha mwaka 2019 hadi mwaka huu, matukio ya ukatili na kutozingatia usawa wa kijinsia yaliyoripotiwa yaliwagusa wanawake 913 na watoto 992 walioathiriwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tangible Initiative for Local Development Tanzania (TIFLD), Geline Fuko, alisema mashirika binafsi yameendelea kupigania haki na sasa kuihusisha teknolojia ya kidigitali kutumika kwenye harakati hizo. "Kutoa taarifa mtandaoni itachangia kutatua matatizo ya ukatili. Katika siku 16 za kupinga ukatili hasa zimejikita kuipigania haki ya wanawake.

"Katika kila wanawake watatu mmoja amepitia ukatili wa kijinsia. Hii ni kwamba wanawake wengi wanahangaika," alisema Geline.

Awali mgeni rasmi, Mkurugenzi wa Shirika la Msaada la Marekani USAID nchini, Kate Somvongsiri, alisema ukatili wa kijinsia unavunja utu wa binadamu na kwamba mfumo wa kidigitali utaongeza uelewa kukabiliana na suala hilo, akisisitiza mamlaka husika kulinda jukwaa la utoaji taarifa na kuwa huru.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya viungo cha Trianon Spices, Edward Rukaka (kushoto), alipotembekea kiwandani hapo katika Kijiji cha Lusanga, wilayani Muheza, mkoani Tanga juzi. Wa (pili kulia) ni Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Halima Bulembo na (kulia) ni Katibu wa CCM wa Wilaya hiyo, Simon Seng'ese. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Waipongeza serikali kwa kuwakumbuka

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NACONGO) limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutambua sekta yao na kuipa fursa ya kuingia kwenye majadiliano ya taifa yanayopelekea kudadavua Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao wao ni miongoni mwa wadau wakubwa.

Mwenyekiti wa baraza hilo, Lilian Badi, alitoa pongezi hizo juzi katika mkutano wa majadiliano ya kimkakati kati ya serikali na washirika wa maendeleo.

Alisema baraza linaishukuru serikali na limeomba ili ushiriki na uhusiano wao uende vizuri, wanahitaji mazingira wezeshi ya kufanya kazi.

"Tuna matatizo kama sekta, tunaona utayari wa kutekeleza mpango wa maendeleo wa miaka mitano sio wa kujadiliana kwa sababu tupo tayari kuutekeleza na tulishaanza na tunafanya miaka yote, matatizo tunayokutana nayo katika sekta yetu tunaomba yatatuliwe," alisema.

Lilian alitaja baadhi ya matatizo hayo kuwa ni uwapo wa sheria ngumu hasa kwenye masuala ya kodi ambazo wanashindwa kuzitekeleza. "Tunashukuru marekebisho yameendelea kufanyika mara kwa mara lakini bado upo uhitaji wa kurekebisha sheria. Kuna utaratibu na uwezeshwaji katika maeneo yetu ya kazi, ukiangalia tunafanya kazi zetu kwenye halmashauri za wilaya, hivyo sekta yetu tunatofautiana viwango.

"Yapo mashirika unapowapa masharti kuwa ni lazima kwa kiwango fulani cha fedha wafike TAMISEMI Dodoma ili kupata kibali, kwao limekuwa suala gumu," alisema. Mwenyekiti huyo aliiomba serikali chini ya Rais Samia isaidie kuondoa matatizo hayo ili mchango wao katika kutekeleza mpango huo uwapo.

Lilian pia alisema wanategemea misaada kutoka nje na wadau wao wanakutana na matatizo ya kupata vibali vya kukaa nchini kwa ajili ya kufanya kazi huku wakiuhitaji utaalamu wao kutekeleza miradi yao.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba alisema kikao hicho cha siku mbili kilichomalizika jana, kiliihusisha serikali na upande wa washirika wa maendeleo, wakiwamo mabalozi wa nchi mbalimbali, wakuu wa taasisi zikiwamo za kifedha.

Alisema vikao hivyo vimelenga kupeana mrejesho wa majukumu ambayo yamekubalika kupitia mpango wa maendeleo na kupeana taarifa ya masuala yanayohusu sera.

# Wanawake walia kunyimwa nafasi nyeti vyama vya siasa

**Na Yasmine Protace**

VIONGOZI wanawake kutoka vyama 19 vya siasa nchini, wamedai mfumo dume uliopo katika baadhi ya vyama vyao umekuwa ukimkandamiza mwanamke ikiwamo kutopata fursa ya ushiriki katika uamuzi.

Hayo yalibainishwa na baadhi ya viongozi wa vyama hivyo kwa nyakati tofauti wakati walipokuwa katika mafunzo ya siku tatu yaliyolenga masuala ya kijinsia katika vyama vya siasa.

Katika mafunzo hayo ambayo yaliratibiwa na Mtandao wa Jinsia (TGNP) kwa kushirikiana na Ulingo, baadhi ya viongozi wa vyama hivyo walisema mfumo dume uliopo katika vyama hivyo unachangia wanawake kushindwa kupata nafasi za juu, hasa katibu au mwenyekiti. Walisema mfumo dume uliopo katika baadhi ya vyama unachangia hata wanawake kukosa nafasi ya ushiriki katika uamuzi.

Waliiomba ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kabla ya kutoa usajili katika vyama, waonyeshwe kwanza katiba za chama kama zinamthamini mwanamke.

Hata hivyo, Dk. Ave Maria Semakafu, Mratibu wa Taifa Ulingo, alisema Sheria ya Vyama imeweka masharti kwa chama chochote kinachosajiliwa lazima kizingatie masuala ya kijinsia.

"Pamoja na kuwapo kwa sheria hiyo, bado baadhi ya vyama viongozi wa juu ni wanaume, hakuna mwanamke. Hali hiyo inachangia haya wanawake kushindwa kufanya uamuzi," alisema.

Aliongeza kuwa kuna kipengele katika katiba kinasema binadamu wote ni sawa, lakini katika hilo la usawa katika vyama linaonekana halipo. Lilian Liundi, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, alisema wapo katika kutafakari kama viongozi wanawake wana uwakilishi katika ngazi za uongozi na kwamba tathmini ya awali inaonyesha hilo bado haijafikiwa.

Aliongeza kuwa inatakiwa kuwapo uwakilishi wa wanawake katika uongozi. Aliongeza kuwa ilani zinasema 50 kwa 50, lakini ilani haisaidii chochote kutokana na kuwapo kwa mapengo.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa kutoka Zanzibar, Mohamed Ally Ahmed, alisema mafanikio ya usawa wa kijinsia Tanzania yatatokana na wanawake katika kupambana wenyewe.

"Sheria iboreshwe ili kuelekeza vyama kumtambua mwanamke katika nafasi za juu za uongozi," alisema.

HABARI KITAIFA

# Kahama wapongezwa kuijali Idara ya Ardhi

**Na Munir Shemweta,** KAHAMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga kwa kuijali na kuihudumia vizuri Idara ya Ardhi tofauti na halmashauri zingine nchini.

Akiwa kwenye ofisi za Idara ya Ardhi katika Manispaa hiyo jana wakati wa ziara ya kikazi mkoani Shinyanga, Dk. Mabula alisema halmashauri hiyo imekuwa mfano kwa halmashauri zingine kutokana na kuijali Idara ya Ardhi kwa kuipatia vifaa pamoja na ofisi kwa ajili ya watumishi wake.

"Ninapenda nichukue fursa hii kumpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na wilaya nzima kwa namna walivyoonesha ushirikiano kwa sekta ya ardhi maana ni halmashauri pekee kulinganisha na zingine kwa kuijali Idara ya Ardhi na kuona kuwa ni sehemu ya halmashauri," alisifu.

Alieleza kuwa ni halmashauri chache zinazoijali Idara ya Ardhi hasa baada ya uamuzi kuhamishiwa wizarani ambapo baadhi ya wakurugenzi walianza kuitenga kwa kudai kuwa siyo sehemu ya halmashauri.

Alisema hali hiyo ni tofauti kabisa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama aliyeamua kutoa ofisi nzuri na kubwa kwa watumishi wa Idara ya Ardhi na kuweka wazi kuwa hata ukiingia ndani ya ofisi hizo unaona hii ni sehemu ya halmashauri.

Dk. Mabula alitoa rai kwa wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuwa Idara ya Ardhi katika halmashauri ni idara kama zilivyo idara zingine na wanao wajibu wa kuihudumia kwa kuipatia vitendea kazi kwa sababu kazi inazofanya ni za halmashauri na inafanya miji ipendeze kwa kuwa halmashauri ni mamlaka ya upangaji.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo alitembelea eneo la viwanda la Zongomela katika Manispaa ya Kahama kujionea namna manispaa hiyo ilivyowapatia eneo wafanyabiashara mbalimbali na kuona kama eneo hilo limezingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Akiwa katika eneo hilo linalojulikana kama Ummy Mwalimu Industrial Park ambalo Halmashauri ya Manispaa ya Kahama imewapatia wafanyabiashra bila malipo, Dk. Mabula aliitaka Idara ya Ardhi kuhakikisha inazingatia mipango ya matumizi ya ardhi katika eneo hilo sambamba na kuwapanga wafanyabiashara kulingana na shughuli zao ili kuepuka mwingiliano.

"Uamuzi wa kuwaleta wafanyabiashra katika eneo hili ni mzuri na napenda niwapongeze lakini ni vizuri mkawapanga hawa wafanyabiashara kulingana na shughuli zao, huwezi kumpanga mama lishe na wanaoranda mbao, hata kiafya siyo nzuri," alisema.

Wafanyabiashara hao mbali na kuishukuru Halmashauri ya Manispaa ya Kahama kwa kuwapatia eneo, waliomba kushughulikiwa kwa kero zinazowakabili katika eneo hilo.

"Mheshimiwa Waziri kwanza tunashukuru kwa kutembelewa na viongozi hapa Zongomela lakini tunaiomba serikali isikilize changamoto zetu ambapo kubwa ni miundombinu ya barabara pamoja na dampo la kutupia taka," alisema mfanyabiashara wa Zongomela aliyejitambulisha kwa jina la Renatus Numbi.



Mratibu wa Mradi wa Kituo cha Umahiri wa TEHAMA (RAFIC), unaotekelezwa na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Joseph Matiko, akizungumza na wahariri na waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali, wakati wa semina ya siku moja kuhusu mkakati wa kutangaza mradi huo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Mkandarasi 'aingia mitini' mkataba wa milioni 194/-

**Ma Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE wa Songwe, Philipo Mulugo, amemjia juu mkandarasi aliyeingia mitini baada ya kupewa zabuni ya kujenga barabara kutoka kijiji cha Kapalala hadi Gua kwa gharama ya Sh. milioni 194.

Imedaiwa kuwa miezi mitatu imepita sasa tangu mkandarasi huyo atie saini mkataba wa ujenzi huo na hajaanza kazi hiyo.

Akizungumza katika kikao cha Bodi ya Barabara juzi, Mulugo alisema mkandarasi huyo wa kampuni ya Yenzebwe Constructions Company Limited ya Mafinga anatia shaka kama ataweza kutekeleza mradi huo na hivyo kuiomba serikali imchukulie hatua au ikiwezekana anyang'anye zabuni hiyo.

"Tatizo ninaloliona ni kubadilishwa kwa sheria ya namna ya kuwapata makandarasi hawa maana wanajaza tenda online (mtandaoni) bila kuwajua sifa zao na uwezo wa vifaa walivyonavyo. Kwa hiyo, ninasema sikubaliani na mwenendo wa mkandarasi huyu," alisema.

Mulugo alisema mkandarasi huyo alitia saini mkataba Septemba 19, mwaka huu kujenga barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 38 lakini tangu atie saini hajafanya kazi yoyote na mvua imeanza na hivyo barabara itakuwa haipitiki.

Aliongeza kuwa ana shaka kama mkandarasi huyo ataweza kumaliza kazi hiyo ndani ya mkataba huo wa miezi sita.

Kufuatia malalamiko hayo ya mbunge, mkandarasi huyo aliitwa jana kwenye kikao katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Songwe kilichohudhuriwa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

Katika kikao hicho, mkandarasi huyo alipohojiwa sababu za kutoanza ujenzi wa mradi, alisema anasubiri mitambo ya kukodi kutoka kwa wenzake ndipo aanze kazi hiyo.

Kufuatia hali hiyo, mkandarasi huyo aliagizwa kufanya haraka kukodi mitambo hiyo iliyopo karibu na eneo la mradi ifikapo Desemba 5, mwaka huu ili aanze kazi ya kujenga barabara hiyo ambayo ni muhimu kwa wananchi wa vijiji sita wanayoitegemea.

# Maandalizi mkutano wa mawaziri EAC yakamilika

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAWAZIRI wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) watakutana jijini Arusha katika mkutano wao wa 41 wa Baraza la Mawairi uliopangwa kufanyika kesho.

Makatibu wakuu wamekamilisha maandalizi yote yanayohitajika kwa ajili ya mkutano huo, zikiwamo nyaraka za taarifa za utekelezaji wa majukumu ya jumuiya, vyombo na taasisi zake katika kikao kilichofayika Novemba juzi na jana.

Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Joseph Sokoine, aliongoza makatibu wakuu wenzake katika kikao hicho, akiwamo Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Prof. Sifuni Mchome; Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais-Ikulu, Zanzibar, Mussa Haji Ali na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah.

Mkutano wa mawaziri ambao utakuwa chini ya uenyekiti wa Kenya na unatarajiwa kufanya uamuzi na kutoa maelekezo kuhusu utekeleaji wa masuala ya mtangamano katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya biashara, miundombinu, afya, ajira, fedha na uanzishwaji wa taasisi mpya hususan taasisi za fedha zitakazosimamia Umoja wa Fedha.

Mawaziri hao pia watapitia na kupitisha ratiba ya shughuli za EAC kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni mwakani.

Kwa mujibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, shughuli hizo zinajumuisha mikutano ambapo kwa kanuni za EAC, asilimia 50 ya mikutano inafanyika katika nchi wanachama na asilimia 50 iliyosalia inafanyika makao makuu ya jumuiya.

Licha ya makao makuu ya EAC kuwa Tanzania, bado nchi hiyo inapewa mgawo wa mikutano ya asilimia 50 inayofanyika katika nchi wanachama.

Mkutano wa mawaziri unatarajiwa kuhitimishwa kwa mawaziri kushuhudia utiaji saini wa mikataba ya utekelezaji wa majukumu (performance contracts) kati ya Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri na Katibu Mkuu wa EAC na baina ya Katibu Mkuu wa EAC na Naibu Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa Idara mbalimbali za EAC.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu kuhusu chanjo corona iendelee kupewa msisitizo

**TANZANIA** ilizindua rasmi chanjo ya corona mwishoni mwa Julai, mwaka huu, ikiwa hatua mojawapo ya kuwakinga wananchi dhidi ya ugonjwa huo ambao umegharimu maisha ya watu wengi duniani ndani ya kipindi kisichozidi miaka miwili.

Tangu kuzinduliwa kwa chanjo hiyo na Rais Samia Suluhu Hassan, tayari Watanzania milioni 1.3 wameshapata chanjo hiyo, ambayo imekuwa ikitolewa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya.

Serikali pamoja na wadau mbalimbali wamekuwa wakihimiza wananchi kupata chanjo hiyo ili kujiweka salama dhidi ya maradhi hayo ambayo taarifa za karibuni zinaonyesha kuwa baadhi ya nchi zimeanza kupata maambukizi kwa awamu ya nne sasa.

Pamoja na idadi hiyo ya watu kupata huduma hiyo kwa lengo la kupunguza makali ya ugonjwa pindi wanapokumbwa nao, hali bado si ya kuridhisha ikizingatiwa kuwa hivi sasa Tanzania inakadiriwa kuwa na zaidi ya watu milioni 60. Kwa mantiki hiyo, kazi bado ni kubwa kufikia malengo yanayotarajiwa kwa nchi ambayo kwa mujibu wa wataalam wa afya ni takriban asilimia 60 hadi 70 ya wananchi.

Wakati hali ikiwa hivyo, jana Mratibu wa Mpango wa Taifa wa Chanjo, Dk. Florian Tinuga, alisema tangu kuanza kwa kampeni ya chanjo, baaadhi ya mikoa imefanya vizuri katika kampeni hiyo ikiwamo Ruvuma, Kagera, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam huku Singida, Songwe na Njombe zikielezwa kuwa zinasuasua.

Hatua hiyo, kwa mujibu wa mratibu huyo, imesababisha serikali kuchukua hatua za kufuatilia ili kubaini vikwazo ambavyo mikoa hiyo inakumbana navyo katika kufanikisha azma hiyo. Licha ya kufuatilia, amebainisha kwamba katika baadhi ya maeneo wananchi wanataka huduma hiyo iwafuate kule wanapoishi au kwenye mikusanyiko na si vituoni ambako chanjo inatolewa.

Hatua hiyo ya baadhi ya watu kutaka kupelekewa huduma, inarudisha nyuma jitihada za serikali kwa kuwa ili kufikia asilimia 60, lengo linalotakiwa ni kuchanja angalau watu milioni 35. Kwa maana hiyo, hata dozi milioni nne ambazo zimeshapitishwa itakuwa ndoto kuzimaliza kama mwenendo utakuwa wa kusuasua hivi.

Ili kufikia lengo na kuokoa maisha ya Watanzania wengi, ni vyema jitihada zikafanyika kuhamasisha wananchi wengi zaidi kupata chanjo. Viongozi wa serikali, kuanzia ngazi za mitaa na vitongoji, wanapaswa kulichukulia suala hilo kama ajenda ya kipaumbele.

Kama alivyosema Rais Samia wakati wa uzinduzi wa chanjo hiyo kwamba suala la chanjo ni kwa usalama wa mtu dhidi ya janga la corona, ni vyema wananchi wakaelimishwa umuhimu wa suala hilo.

Ni wazi kwamba katika baadhi ya maeneo watu wametawaliwa na mila potofu jambo ambalo linasababisha wengi kutokujitokeza kuchanjwa. Katika eneo hilo nguvu zaidi inatakiwa ili watu wajitokeze kwa wingi.

Jambo la msingi na muhimu kwa Watanzania ni kwamba jamii haipaswi kusubiri mpaka kukumbwa na janga ndipo ianze kuchukua hatua. Tumeshuhudia katika mambo mengi watu hawataki kuchukua hatua za kujikinga hadi waugue ndipo waopate matibabu, jambo ambalo ni hatari kwa ustawi wa jamii.

Kama wahenga wasemavyo heri kuzuia kuliko kutibu, ni vyema Watanzania ambao hawajachukua hatua ya kuchanja, wakafanya hivyo ili kujiokoa na kujilinda dhidi ya maradhi pamoja na vifo ambavyo vinaweza kuzuilika kwa sababu tu ya kinga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Elimu na uhamasishaji vitahitajika zaidi kwa ajili ya chanjo ya corona

Na Sabato Kasika

**TANGU** Rais Samia Suluhu Hassan azindue rasmi kampeni ya chanjo ya corona mwishoni mwa Julai, mwaka huu, tayari Watanzania milioni 1.3 wameshapata chanjo hiyo, katika maeneo mbalimbali nchini.

Hiyo ndiyo idadi hiyo ya Watanzania waliojitokeza kupata chanjo katika vituo mbalimbali, kuanzia siku ambayo Rais alizindua kampeni hizo Julai 29, mwaka huu, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Miongoni mwao wamo 988,293 ambao ni sawa na asilimia 1.7 ya Watanzania, wamekamilisha chanjo na kupata kinga kamili dhidi ya ugonjwa huo, kwa chanjo moja ya Jensen na wengine dozi mbili ya Sinopharm. Lakini pia kuna wengine 371,331 ambao ni sawa na asilimia 0.6 ya Watanzania, wamechanja dozi moja ya Sinopharm na wanasubiri chanjo nyingine ili nao wakamilishe dozi yao.

Mikoa 10 ikiwamo ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Dodoma, Arusha, Mwanza, Ruvuma, Mbeya, Morogoro, Mtwara na Kagera, ndiyo ambayo inatajwa kuongoza katika utoaji wa chanjo.

Mbali na idadi ya watu waliochanjwa, Tanzania pia imeshapokea dozi 1,227,400 za Jensen za kukinga watu 1,227,400 kwa dozi moja na dozi 2,578,400 za Sinopharm za kukinga watu 1,289,200 kwa dozi mbili.

Hizo ni takwimu zilizotolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akipokea chanjo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Dar es Salaam.

Sasa ni zaidi ya miezi mitatu tangu kampeni ya chanjo izinduliwe, lakini idadi ya waliochanjwa ninaona kama bado ndogo, hivyo ninadhani ipo haja ya kuongeza kasi ya utoaji wa elimu na uhamasishaji kwenye jamii.

Elimu na uhamasishaji vinahitajika, kwa sababu suala la chanjo liliingiliwa na wataalamu wa mitaani ambao nao wamekuwa wakitoa elimu yao ambayo inaweza kuchangia baadhi ya watu kutojitokeza kwa wingi kuchanjwa.

Pamoja na hilo, kuna methali isemayo; 'umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu', inaweza kuwa sawa na kidole kimoja hakivunji chawa, jiwe moja haliinjiki chungu, ikimaanisha kuhimiza ushirikiano, ili kufanikisha jambo kwa pamoja.

Hata kwenye suala hili la chanjo, ushirikiano ni wa muhimu, kwani vinginevyo inaweza kuwa vigumu kufikia lengo, hivyo ingekuwa vizuri iwapo jamii inashirikiana na serikali kuhimiza watu kujitokeza kuchanjwa.

Kila mara serikali imekuwa ikihimiza wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini kushirikiana nayo katika kupambana na ugonjwa huo, kwa kuwa ni vita ambayo kila mmoja anahusika.

Serikali inahimiza hilo, kutokana na ukweli kwamba, viongozi wa dini wana mchango mkubwa katika kuhamasisha waumini kuchukua tahadhari, lakini pia kuwaambia wajitokeze kupata chanjo katika vituo mbalimbali.

Iwapo watajitokeza watu na kusema hawawezi kushiriki katika vita dhidi ya ugonjwa huo, kwa madai kwamba si kazi yao, wanaweza kukwamisha juhudi zinazofanywa na serikali za kutaka ugonjwa huo unatoweka nchini.

Kwa kuwa chanjo ni hiari, ingependeza kama hatakuwepo mtu wa kumshawishi mwingine asichanjwe. Kila mmoja aachwe aamue, kwani suala la usalama wa afya yake linamhusu mwenyewe.

Nimegusia hilo kwani hivi karibu iliripotiwa kwenye vyombo vya habari kuwa baadhi ya wanaume, katika Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, walikuwa wanawazuia wake zao kwenda kupata chanjo, kwa madai kwamba si salama.

Watu hao nao ni vyema kama wataelimishwa na kumbushwa kuwa, miongoni mwa hatua iliyochangia kwa kiasi kikubwa kupunguza maambukizi na visa vipya vya UVIKO - 19 duniani, ni chanjo mbalimbali.

Hivyo ni vyema jamii ikajitokeza kwa wingi kupata chanjo, kwani hatua hiyo inaelezwa kuwa inasaidia kupunguza milipuko, ambayo inaweza kutokea mara kwa mara hasa kwenye ugonjwa mkali unaohitaji matibabu ya muda mrefu.

Kimsingi ni kwamba, Watanzania wasikubali kugawanyika katika vita dhidi ya corona, badala yake watoe ushirikiano kwani ndiyo njia mojawapo ya kuhakikisha kila anayetakiwa kuchanjwa anapata chanjo.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Kampuni ya TotalEnergies imeonyesha kile kinachotakiwa katika uwekezaji



Na Pascal Mayalla

**Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyekuwa mgeni rasmi, kwenye uzinduzi wa vilainishi vipya vya magari na mitambo vya TotalEnergies, uliofanyika jana jijini Dar es Salaam uliokwenda sambamba na maadhimisho ya wiki ya wateja wa TotalEnergies, alipongeza kampuni hiyo kwa uamuzi wa kuzalisha vilainishi hivyo na kuisaidia nchi kutokuagiza nje.**

TANZANIA ni nchi inayopiga hatua mbalimbali za kimaendeleo na imefungua milango yake kutoa fursa za uwekezaji kutoka wawekezaji mbalimbali, ambao si tu wanaleta mitaji kupitia miradi ya uwekezaji ya moja kwa moja (FDI) bali pia wanaleta teknolojia na wataalamu kutoka nchini kwao kuja kufanya kazi.

Kampuni ya mafuta ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, moja ya kampuni zilizokuja nchini zaidi ya miaka 50 iliyopita, kwa sasa ndiyo kampuni inayoongoza kwa uwekezaji toka tumepata uhuru.

Mradi wake wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania, ndio mkubwa kabisa wa uwekezaji kuliko wowote nchini.

Wawekezaji wengine karibu wote, si tuu huwa wanaleta mitaji bali pia huleta mitambo na wataalamu wao kuja nchini lakini kwa TotalEnergies, ni tofauti kidogo. Badala ya kuleta wataalamu kutoka kwao, wanakwenda kwenye vyuo vikuu vya nchini kuvuna vijana wenye akili na kuwapika kwa kuwasomesha na mafunzo ya utaalamu, hivyo kulijengea taifa uwezo wa kitaalamu.

Kwa mantiki hiyo, kazi za kitaalamu zinafanywa na wataalamu Watanzania waliojengewa uwezo.

Wiki iliyopita, kampuni hiyo ambayo awali ilijulikana kama Total Tanzania Limited, ilizindua Wiki ya Huduma kwa Wateja ya TotalEnergies kwa mwaka 2021 yenye kaulimbiu ya "Tuijenge Kesho Pamoja" hii ni awamu ya tatu ya wiki ya huduma kwa mteja kwa kampuni hiyo tangu mwaka mwaka 2019.

TotalEnergies inaendelea kuonyesha dhamira yake kwa Tanzania kwa kuwakaribisha wateja wao ili kushiriki maono yao ya mustakabali wa kampuni.

Kutokana na utaratibu huo wa kuwajengea uwezo wenyeji ndipo ulete mtaji, serikali imeipongeza kampuni hiyo kwa kuunga mkono juhudi za Tanzania kujenga Tanzania ya viwanda kwa kujenga viwanda, kutoa ajira, na kuleta teknolojia kwa Watanzania.

Kabla ya ujenzi wa kiwanda cha vilainishi, Tanzania ilikuwa inaagiza nje kwa sababu tulikuwa hatuna kiwanda cha kutosheleza soko. Lakini sasa kupitia TotalEnegies, Tanzania inajitosheleza kwa vilainishi na ziada tutauza nje.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyekuwa mgeni rasmi, kwenye uzinduzi wa vilainishi vipya vya magari na mitambo vya TotalEnergies, uliofanyika jana jijini Dar es Salaam uliokwenda sambamba na maadhimisho ya wiki ya wateja wa TotalEnergies, alipongeza kampuni hiyo kwa uamuzi wa kuzalisha vilainishi hivyo na kuisaidia nchi kutokuagiza nje.

Naibu Waziri alisema vilainishi hivyo vinatumia teknolojia ya kisasa kuvitengeneza lakini licha ya kufanya biashara, vitawajengea uwezo Watanzania si tu kwa kupatiwa fursa za ajira bali uwezo wa uhawilishaji teknolojia kutoka kwao, kuileta Tanzania.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mkurugenzi Mkuu Jean-Francois Schoepp, alisema: "Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema kuwa ikiwa maendeleo ya kweli yatatokea, ni lazima wananchi washirikishwe, tunaamini kwamba TotalEnergies itaendelea kukua zaidi endapo tutawashirikisha wateja wetu na kuwa tayari kukidhi mahitaji kikamilifu."

Wafanyakazi wa TotalEnergies, wakiongozwa na Schoepp walitoa huduma kwa wateja waliotembelea kituo cha TotalEnergies East Oysterbay siku ya Jumatatu na kupata fursa ya kusikiliza maoni ya wateja, kuboresha uhusiano na wateja wao kwa nia ya kuziba mapengo yoyote yaliyokuwapo na kujenga TotalEnergies kwa pamoja na wateja wao.

Zaidi ya hayo, wateja walipata nafasi ya kucheza gurudumu la bahati katika kituo hicho na walijishindia zawadi kadhaa zikiwamo fulana, chupa za maji, kofia, bidhaa za kutunza magari kama vile baridi na air freshener, na vocha ya zawadi zilizowawezesha kununua bidhaa zozote katika duka la Cafe Bonjour lililoko kituoni hapo.

Bila shaka, TotalEnergies imekuja na taswira mpya na kuwa wabunifu zaidi.

Hii inaakisiwa kikamilifu na ushirikishwaji wa wateja kwa nia ya kuboresha bidhaa na huduma zao ili kukidhi mahitaji ya kila Mtanzania anayehitaji huduma za mafuta, vilainishi na bidhaa zipatikanazo madukani.

Hakika, TotalEnergies Marketing Tanzania Limited imekuja na taswira mpya na kuendelea kuwa kampuni inayoongoza kwa ubora. Hii inaonekana kikamilifu katika dhamira yake ya kutoa bidhaa na huduma bora kila mahali nchini Tanzania.

**Pascal Mayalla**
**+ 255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tanzania yangu mbona inanichanganya?



Na Joseph Kulangwa

**"Yaani toto la kike lipate mimba halafu liendelee na masomo! Labda si mimi!" Tukashangilia, wakaingia Wazungu kutukejeli na kutubeza huku wakitishia kutunyima njuluku, tukasimama na kiongozi wetu na kuwasema huku tukijifanya masikini jeuri kwamba hatutasomesha kina mama.**

HII ndiyo Tanzania yetu. Ni nchi ya amani na utulivu na yenye watu wanaopendana na wenye mshikamano wa hali ya juu. Lakini mimi naona nachanganyikiwa. Lakini nachanganyikiwa kisiasa zaidi.

Miaka michache iliyopita, tulikuwa na mambo mengine na hivi sasa tuna mengine. Kuna yaliyotokea enzi hizo yakatushangaza tukashangaa. Mengine yakatufurahisha tukafurahi. Ndivyo ilivyokuwa.

Tulikuwa na kiongozi shujaa na jasiri akafanya yake mazuri na mabaya akaondoka. Tukamuaga na sasa tunamkumbuka kwa aliyoyafanya hususan mazuri. Alijenga miundombinu ambayo hivi sasa tunaishuhudia. Miradi ya kimkakati tunaiona.

Alikataa kabisa kujengwa kwa bandari Bagamoyo akatoa sababu zake zikiwamo za kutaka kutupiga kijanja. Tukashangilia kuanzia nje mpaka bungeni. Tukaamini tunataka kupigwa na kina 'machodogo'. Ikapita.

Akahoji kuhusu chanjo ya UVIKO-19, akahadharisha kuwa tusiikimbilie kwa sababu haikufanyiwa utafiti kwa muda wa kutosha. Akasema wanataka kutumaliza hawa wenzetu. Tuwe makini.

Alitangaza elimu bure kwa kila mtoto mwenye umri wa kwenda shule. Lakini akasema kamwe katika utawala wake hatakubali kuona tukisomesha kina mama. "Yaani toto la kike lipate mimba halafu liendelee na masomo! Labda si mimi!"

Tukashangilia, wakaingia Wazungu kutukejeli na kutubeza huku wakitishia kutunyima njuluku, tukasimama na kiongozi wetu na kuwasema huku tukijifanya masikini jeuri kwamba hatutasomesha kina mama.

Kwenye UVIKO-19 huko, tukawa tukimwona kiongozi wetu, tunavaa barakoa na kuzificha tukichelea kuzodolewa na kuvaa mibarakoa. Tukaanza kujifukiza kwa kwenda mbele, kila mtu na nyungu yake.

Wabunge na mawaziri wakaacha kazi zao na kuhamia kwenye nyungu, wakihanikiza kila mahali mpaka wengine wakaanza kupiga picha na familia zao wakijifukiza, huku tukijenga vibanda vya 'Tigo Pesa' na 'M-Pesa' hospitalini kujifukiza.

Mh! Alipoondoka tu mpendwa wetu, tumebadilika tulipoingia enzi za Chifu Hangaya. Masikini kutokana na upendo alionao Chifu wetu akawabakiza wale wale waliokuwa kwa Mtemi Magu. Wale waliokuwa wakishangilia matamko yake.

Leo unawaona wakiwa chini ya Chifu Hangaya wanatubadilikia ghafla na kuwa kana kwamba hawakuwa wale wa miaka mitano sita iliyopita. Ndio wanaounga mkono ujenzi wa bandari ya Bagamoyo tena nje na ndani ya Bunge.

Ndio hao hao leo tunawaona wanakimbilia barakoa na kuacha kabisa nyungu, na sasa tuko nao tukihanikiza chanjo ya Uviko-19. Tunahanikiza nao kudungwa JJ na Faiza. Ndio hao leo wanahanikiza kwamba binti ukiwa shule ukatundikwa mimba zaa rudi.

Kinachonichanganya mimi sasa, ni kuona wale wale waliokuwa wakikubaliana na yote ya Mtemi Magu, ndio hao hao leo wanayakataa yale ya Mtemi na kubadilika kabisa. Nachanganyikiwa kwa kweli.

Pengine Chifu Hangaya angekuja na timu mpya ili tusione vinyonga katika Serikali yake, mambo yangekuwa mazuri, tusingechanganyikiwa kama nilivyojikuta miye. Najiuliza huyu aliyepinga ndiye huyu huyu anayekubali?

Najiuliza hivi kumbe mtu anapoamua jambo anaamua kwa sababu ya nafasi na si kwa sababu ya imani, si kwa kuwa anaamini kwamba anachokiamua ndicho kinaweza kumsaidia Mtanzania?

Jana unasema bandari ya Bagamoyo haifai. Leo unasema inafaa, halafu ni ile ile na iko pale pale! Jana ukasema chanjo ya UVIKO-19 haifai, lakini leo unahanikiza kuwa ndiyo yenyewe na kutaka sasa ichanjwe, tena bila hiyari.

Wewe huyo, jana ukakasirika kusikia watu wanaoendekeza mtoto wa kike kupata mimba shuleni, aachwe akajifungue kisha kijukuu amwachie mama yake arudi shule kuendelea na masomo ili atimize ndoto yake.

Leo wewe huyuhuyu unaibuka na kusema hiyo ni haki ya binadamu, mtoto wa kike kujifungua na kurejea kwenye masomo yake kama awali. Hivi nani sasa wa kulaumiwa hapa? Watu, muda, wakati au muktadha?

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Wananchi Ngorongoro tumieni busara kwa kuchagua mbunge



Na Thobias Mwanakatwe

KATIBA ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeainisha haki ya kupiga kura katika Ibara ya 5 (1) ambayo inaeleza kuwa; Kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18, anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi.

Na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya ibara ndogo ya (2) pamoja na masharti mengineyo ya katiba hii na sheria inayotumika nchini Tanzania. Desemba 11, mwaka huu, wananchi wa jimbo la Ngorongoro mkoani Arusha, wanatarajia kushiriki kupiga kura katika uchaguzi mdogo wa ubunge.

Uchaguzi huo unafanyika kutokana na kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), William Tate Ole Nasha, aliyefariki dunia Septemba 27, mwaka huu. Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ambayo kisheria ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi huo, tayari imeshateua wagombea 11 kutoka vyama mbalimbali vya siasa kuwania nafasi hiyo.

Wagombea hao tayari wameshaanza kampeni tangu Novemba 16, mwaka huu, ambazo watazihitimisha Desemba 10 na siku itakayofuata itakuwa hukumu kutoka kwa wananchi ambao watapiga kura kumchagua mmoja kati ya wagombea hao kuwa mbunge wao.

NEC kwa kutambua tatizo, kila uchaguzi ukiwamo uchaguzi huu wa Jimbo la Ngorongoro, imekuwa ikijitahidi kuwaelimisha wananchi umuhimu wa wao kushiriki kupiga kura.

Katika uchaguzi mdogo wa Ngorongoro, tayari maofisa 12 kutoka NEC wamejichimbia jimboni humo kuwapiga msasa wananchi ili watambue umuhimu wao katika kushiriki kupiga kura.

Maofisa hao wa NEC wanawaelimisha wananchi pamoja na mambo mengi kuwakumbusha tarehe ya kupiga kura, kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura na jinsi ya kupiga kura ili kupunguza idadi ya kura zinazoharibika kutokana na baadhi ya wapigakura kutokuwa na uelewa mzuri.

Elimu ya mpigakura inatolewa kwa wakazi hao kwa njia ya ana kwa ana katika kaya, mikusanyiko mbalimbali kama mikutano ya koo, vitongoji , kata na maeneo zinapofanyika shughuli za kijamii kama biashara, malisho, majosho na vikoba. NEC imepewa mamlaka ya utoaji wa elimu ya mpigakura kupitia kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343.

Elimu ya mpigakura inalenga kuwahamasisha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba katika kujitokeza na kushiriki kuchagua viongozi watakaowaongoza ili kujenga demokrasia na utawala bora.

Dhana hii ya elimu ya mpigakura inahusisha pia usambazaji wa taarifa, vielelezo na vipindi mbalimbali katika vyombo vya habari ambavyo vinalenga kuwaelimisha wananchi juu ya mchakato wa uchaguzi.

Mchakato huu huwa unahusisha uandikishaji wa wapigakura, ugawaji wa majimbo, uwekaji wazi daftari la wapigakura, kampeni, utaratibu wa kupiga kura na vituo vya kupigia kura.

Elimu ya mpigakura hutolewa kuhakikisha wapigakura wanahamasika na wanakuwa tayari kwa hiari yao, kwa ufahamu wao na kwa kujiamini kwao, kushiriki katika mchakato wa uchaguzi wakiwa na mtizamo wa kukuza demokrasia.

Lakini pia umuhimu wa elimu ya mpigakura ni nyenzo na kielelezo muhimu katika kumuwezesha kila mwananchi kuelewa kuhusu mchakato wa Uchaguzi na nafasi yake katika kupiga kura. Elimu hii huwajengea ufahamu wananchi kuhusu haki na wajibu wao kushiriki katika mchakato wa uchaguzi wakiwa na taarifa kamili na sahihi juu ya michakato yote ya uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani.

Kwa msingi huo, wananchi wa Ngorongoro na Watanzania kwa ujumla, lazima wafahamu kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa wao kushiriki kupiga kura kwa kuwa mwananchi anapofanya hivyo anakuwa ametimiza haki yake ya kikatiba ya kushiriki katika ujenzi wa maendeleo ya nchi na upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na kiuchumi kwa faida yake na vizazi vijavyo.

Wananchi wa Ngorongoro lazima mfahamu kuwa kura inatoa fursa kwa wananchi kunufaika na matumizi ya kodi mnazolipa na kura ikitumika vizuri inaweza kutatua matatizo ndani ya jamii.

Naishukru NEC ambayo imeamua kujichinbia Ngorongoro kwa ajili ya kutoa elimu kwa wapigakura, pengine hili litasaidia kuwatoa 'tongotongo' wale wanaodhani kuwa suala la kupiga kura halina maana.

Siku ya kupiga kura, mwananchi wa Ngorongoro kabla hujachukua uamuzi lazima uyatafakari maneno, kauli, ilani na sera ambazo mgombea husika na chama chake walikuwa wakiyanena kwenye mikutano yao ya kampeni.

Na hapa ndipo unatambua kuwa kipindi cha kampeni ni cha muhimu kwa wananchi kusikiliza sera za wagombea kwa sababu hapo ndipo unapata kufahamu mgombea mwenye malengo ya dhati ya kukuletea maendeleo ni nani.

Ni matumaini ya kila mwananchi atapata fursa ya kuwasikiliza wagombea wote, na niweke wazi wapo baadhi yao sera na mipango yao inatisha kidogo kwa mustakabali wa jimbo na nchi kwa ujumla. Sina haja ya kuwaelezea wagombea hao.

WanaNgorongoro twendeni tukapige kura tukizingatia kuwa tunakwenda kuchagua viongozi sahihi na makini watakaotuletea maendeleo ya kweli na siyo wenye lengo la kuvuruga amani yetu.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA,**
**MUNGU IBARIKI NGORONGORO**
**mwanakatwe2005@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# HILI NDILO SULUHISHO LA MIGOGORO, KUVUNJIKA KWA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

NDOA ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu na kitovu cha familia, jamii, taifa na malezi. Taasisi hii ya ndoa inahitaji matunzo na malezi. Kwa kuzingatia ukweli huo, familia kama chimbuko la uhai na uzima, shule ya upendo, maadili, imani na uwajibikaji ni mahali ambapo kila mmoja anapaswa kujifunza mambo mema ili kuwa na msingi imara wa maisha yake.

Kwa msingi huo, ndoa zikiwa imara, taifa linakuwa imara, kwani wananchi na viongozi mbalimbali katika jamii wanatoka katika familia.

Ndoa nyingi za siku hizi hazina msingi imara na nyingi zimepoteza mvuto kwa sababu ya kukosa malezi na matunzo. Wanandoa wengi wamekuwa wanaharakati zaidi kuliko kuwa walezi wa ndoa zao kiasi cha kusababisha maumivu na majeraha ya nafsi miongoni mwao. Mungu alianzisha taasisi ya ndoa ili watu waingie, waipende na kuifurahia.

Hata hivyo, inasikitisha kwamba, kwa baadhi ya familia, ndoa imegeuka kuwa jela ya nyumbani hivyo kusababisha upotoshwaji mkubwa juu ya kusudi na maana halisi ya ndoa na familia.

Kumekuwa na ongezeko kubwa la migogoro na kuvunjika kwa ndoa nchini. Baadhi ya ndoa zimedumu kwa muda mfupi chini ya mwaka mmoja. Mkoa wa Dar es Salaam umetajwa kuongoza kwa uwingi wa mashauri ya ndoa na talaka nchini. Kwa kuzingatia hotuba ya Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahimu Juma, aliyoitoa jijini Dodoma hivi karibuni, pamoja na mambo mengine, alibainisha kwamba kati ya mwaka 2017 na 2019, kulikuwa na mashauri ya ndoa takribani 4,200 na mirathi 7,600 katika mahakama Dar es Salaam. Takwimu za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) zinaonyesha kuwa kwa mwaka 2020/21 RITA imesajili talaka 551 nchini na kwamba idadi hii inazidi kuongozeka kwa kasi.

Ni dhahiri kuwa wanandoa wengi wamepoteza hisia chanya na mvuto miongoni mwao. Kuvunjika kwa ndoa ni msamiati unaoanza kuzoeleka na kuonekana kuwa ni mtindo wa maisha kisasa, jambo ambalo si sahihi. Hiki ni kiashiria kwamba ndoa nyingi zinahitaji ukarabati na matengenezo. Kwa uzito huo huo, mafundisho yakinifu kuhusu taasisi ya ndoa yanahitajika kwa wanandoa watarajiwa ili wafahamu kwa undani juu ya yawapasayo kabla ya kuingia katika ndoa na kuyaishi maisha ya ndoa baada ya kuoa na kuolewa.

Athari za migogoro na kuvunjika kwa ndoa ni kubwa. Kwa kutaja kwa uchache, migogoro na kuvunjika kwa ndoa huondoa hisia za mapenzi na mvuto. Matokeo ya hali hii ni kuongezeka kwa vitendo vya ukatili na unyanyasaji ndani ya ndoa (domestic Violence) na matukio ya wanandoa/wapenzi kuuana. Uzoefu unaonyesha kuwa, waathirika wakubwa wa vitendo hivi ni wanawake na watoto.

Athari za migogoro na kuvunjika kwa ndoa haziwahusu wanandoa tu, bali pia wazazi ambako wanandoa hao wanatoka kwani huleta masononeko na uadui wa kifamilia. Athari za migogoro na kuvunjika kwa ndoa ni kubwa zaidi kwa watoto kwa kuwa huathiri makuzi yao, watoto wanakosa haki ya kuishi na wazazi wote wawili na kusababisha mmomonyoko wa maadili. Migogoro na kuvunjika kwa ndoa huleta msongo wa mawazo wenye athari mbaya (stress-leading to negative effects) kiroho, kiuchumi, kisaikolojia, na kiafya na kuvuruga mfumo wa maisha.

Zaidi sana, migogoro na kuvunjika kwa ndoa huathiri ufanisi wa utendaji kazi na kupunguza uzalishaji; ongezeko la familia za mzazi mmoja, ajira na mimba za ututoni, watoto wa mitaani na uhalifu. Hivi karibuni, imetolewa taarifa katika vyombo vya habari kuwa, huko Tanga kuna kundi la watoto linalojiita "watoto wa ibilisi"ambalo hufanya vitendo vya kihalifu. Hali hii si kiashiria kizuri kwa usalama na maendeleo ya taifa.

Kwa kuzingatia ongezeko la migogoro, mashauri ya ndoa na talaka nchini, asasi ya Tanzania Marriage and Chaild Care (TaMCare) Foundation hivi karibuni ilizindua programu maalum ya pekee nchini yenye jina, Kliniki ya Ndoa na Uhusiano (Marriage and Relationship Clinic) ikiwa ni njia ya kushirikiana na serikali na wadau wengine nchini nchini katika kukabiliana na tatizo la migogoro na kuvunjika kwa ndoa ili kupunguza talaka, vitendo vya ukatili wa kijinsia na kasi ya mmomonyoko wa maadili katika jamii. Uzinduzi wa Kliniki hii, ni mwarobaini wa matatizo hayo yaliyotajwa.

Matatizo mengi yanayoikabili jamii yetu chanzo chake ni tabia. Ni dhamira ya TaMCare kulinda, kuokoa tabia, maadili na mwenendo wa watoto, vijana, wanandoa na watu wote kwa ujumla ili kujenga familia na taifa lenye maadili mema. Maadili mema ni uhai kwa familia na taifa. Hatuwezi kuendelea kiroho, kimwili, kiuchumi, kisiasa na kijamii pasipokuwa na maadili yanayompendeza Mungu na binadamu wenzetu.

Tabia ndiyo chanzo cha matendo tunayoyaona. Mathalani, kukosekana kwa uaminifu, ubadhirifu wa mali za umma, ufisadi, migogoro ya ndoa, misuguano ya kijamii, ugaidi, ukatili, unyanyasaji, na unyanyapaa na kadhalika. Kliniki hii ya Ndoa na Uhusiano iliyozinduliwa imezingatia ukweli kwamba familia ndiyo msingi wa maadili mema katika jamii na taifa. Maendeleo yoyote yanahitaji watu waadilifu.Uadilifu huo unajengwa kuanzia ngazi ya familia.

Katika kliniki hii, jamii itaelimishwa kuhusu masuala yanayohusu ndoa na uhusiano ili kujenda uhusiano bora miongoni mwa wanandoa na kutokomeza vitendo vya ukatili, unyanyasaji na mauaji ya wanandoa; kuelimisha jamii kuhusu talaka na mirathi; afya, lishe na malezi bora ya watoto ili kuimarisha afya ya akili, mwili na uhusiano; kutoa elimu ya kujitambua na maarifa ya nyumbani kwa vijana ili ndoa zao zidumu na kuwa baraka badala ya karaha.

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

NOVEMBA 28, 2021
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili



Ukurasa 14

## JIPE RAHA NA UBUYU



Ukurasa 15

## NYUMBA:

Dondoo za usafi wa bafu na choo


12 MAISHA JUMAPILI NOVEMBA 28, 2021

HARUSI

HARUSI

Ukurasa 12





KICHEKO MURUA

## Meno meupee yanayong'ara

Ukurasa 14

MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | N | Y | A | M | A |
| ■ | Y | ■ | ■ | W | ■ |
| B | A | A | ■ | A | ■ |
| ■ | N | ■ | U | M | A |
| ■ | Y | ■ | ■ | B | ■ |
| K | A | T | W | A | ■ |

## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | | | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | ■ | | ■ |
| ■ | | ■ | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | | | ■ |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IMO, HAI, LAMBA, TANGA, TIMIZA, GAWANA

## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO John alikuwa subuleni akiangalia kipindi cha wanyama, alifurahi sana kuwaona simba, twiga, nyati na nyumbu. Alimuona simba dume akiunguruma kwa sauti nene ambayo ilisababisha wanyama wengine kukimbia.

Baada ya kuona hivyo, alimuuliza mama yake kuhusu mnyama simba.

John: Mama hivi huyu simba anayeunguruma anapata chakula wapi?

Mama: Anapata chakula chake kwa kuwawinda wanyama wengine kama swala, nyati na nyumbu

John: Anapataje wanyama wakati mwalimu katuambia kwamba simba mwenda kimya ndiye mla nyama?

Mama: Mwanangu huo ni mzemo tu, una maana kwamba kila unapofanya jambo kwa utaratibu, utapata mafanikio na sio vinginevyo.

SWALI
Taja maana zaidi ya moja neno 'Mto'

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mchumba aliyekukataa anapogeuka mlinzi wako

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu za Maisha Ndivyo Yalivyo. Bado tunajadili shuhuda za watu waliopoteza nafasi zao.

Tayari tumemuona mfalme Nebukadneza aliyepoteza nafasi aliyopewa na Mungu akajikuta anaishi na wanyama msituni kwa miaka saba. Tukaona pia kijana aliyefanikiwa kujenga ghorofa kijijini kwao lakini Sh. 5,000 aliyompa mjomba ambaye naye aliipeleka kwa mganga wa kienyeji, ilimrudisha kijana kwenye umasikini.

Alijenga ghorofa, akajikuta anaiuza aweze kukomboa makontena bandarini. Vyote hivyo havikuwezekana akafilisika. Kisa mjomba hakutaka awazidi watoto wake kwa mafanikio.

Mpenzi msomaji, Mungu akikupa nafasi, iwe ndogo au kubwa, itumie kujenga ufalme wake na ndipo yeye atakuongezea hicho ulicho nacho. Na akikupa nafasi akaona unaichezea, anaihamishia kwa mtu mwingine.

Yapo maneno ya Mungu yanasema; 'kwa maana imeandikwa, kikao chake na kiwe ukiwa, wala asiwepo mtu wa kukaa humo, tena usimamizi wake autwae mwingine'. Ukilegea katika nafasi yako unayosimamia, usipokuwa makini atapewa mwingine na hiyo inaanzia kwenye ulimwengu wa roho.

Hebu sikia ushuhuda mwingine. Dada mmoja alichumbiwa na mwanajeshi. Maandalizi ya harusi yalipokamilika akawa na usongo sana wa kuolewa. Akajiandaa mapema siku hiyo asubuhi akawahi kanisani.

Ilipofika saa nne akaanza kuwa na wasiwasi mbona bwana harusi mtarajiwa haonekani. Akajitia moyo kuwa atakuja lakini wapi. Kufika saa sita akaanza kulia na hadi saa saba hakuna mchumba.

Shela ya harusi ikachafuka kwa machozi na rangi za poda (make-up) zikavurugika, jasho jembamba likamtoka. Ilibidi kiongozi wa dini aliyekuwa aifunge ndoa ile akaiahirisha kwa mujibu wa sheria ya ndoa.

Dada akaondoka amekasirika na shela lake. Baada ya miezi mitatu akaamua kusamehe yote yaliyotokea. Yule mchumba wake hakutokea tena hata mawasiliano kwa simu hayakupatikana tena.

Dada akamwambia Mungu anasamehe yote. Na kanuni ya Mungu unaposamehe na kumuondoa mtu moyoni, naye huanza upya na wewe. Baada ya mwaka mmoja, yule dada akachumbiwa tena na mwanajeshi. Safari hii hakuwahi tena kanisani akihofiwa kukataliwa tena. Akafika kanisani saa tano asubuhi na bahati nzuri bwana harusi mtarajiwa naye akawasili. Dada hakuamini na ndoa ikafungwa saa saba. Baada ya mwaka mmoja mumewe huyo akapandishwa cheo na kuwekewa mlinzi.

Baada ya kupewa mlinzi alimjulisha mkewe. Alipomchungulia tu nje akagundua kumbe mlinzi ni yule mchumba aliyemuacha solemba siku ya harusi. Dada kichaa kikaamka upya akawa mbogo. Akamwambia mumewe kuwa huyo mlinzi ndiye aliyemdhalilisha siku ya harusi hakutokea kanisani ndoa ikafa.

Mwanajeshi kusikia vile akamwambia mkewe, kama huyu ndiye aliyekudhalilisha basi mimi simtaki, nakupa awe mlinzi wako (bodigadi) wako. Yule dada akasema sawa, nitamuonyesha shoo hadi ataharuki.

Dada akaanza, siku ya kwanza akamwambia mlinzi, "samahani, nishikie mkoba kidogo". Siku nyingine dada akawa anaingia chooni, akamwamuru asiondoke hapo mlangoni. Wakati mwingine anamwambia amrekebishe poda usoni, ili mradi tu amkomeshe.

Msomaji wangu, Mungu akikuinua siku moja nenda kule walikokudharau. Kawaonyeshe kuwa Mungu huinua, hubadilisha. Mungu akishakupa hakuna wa kukunyang'anya. Acha maadui zako wageuzwe kuwa walinzi wako. Kuna mahali watakukuta, wataona aibu.

Kijana aliyemuacha binti siku ya kufunga ndoa, Mungu alimpa nafasi ya kuoa, lakini ikamponyoka. Sasa anajikuta anarudi kwa yule mchumba kwa jukumu lingine la ulinzi.

Wapo watu wengi wanajutia leo baada ya familia zao kusambaratika. Kisa walipuuzia dalili mbalimbali zilizokuwa zinaonekana katika maisha yao ya kila siku.

Kwa mfano, baba aliyekuwa akitoa maamuzi akasikilizwa na familia yake, leo mke na watoto hawamsikilizi, wanamdharau. Ukiona hivyo, tayari ameshatolewa kwenye nafasi yake kama baba. Huyu anapaswa kuwa kichwa siyo mkia.

Ukiona mama anachukua nafasi ya baba, hiyo familia lazima itayumba tu. Ipo tahadhari ya kimungu kwamba, 'usimwachie mwanamke ukuu wako...' Huyu ni baba anaambiwa. Ukimwona mwanamke anakuwa ni mtoa uamuzi badala ya baba, tayari baba ameshatolewa kwenye nafasi kitambo.

Ukiona mama anashikamana na watoto kumpiga vita baba, huyu ameshapinduliwa. Hii ni hatari sana nyumba haitakuwa na amani kwani familia imegawanyika.

**Msomaji, bila shaka umejifunza kitu hapo. Shuhuda zitaendelea wiki ijayo. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe mfupi 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Ufafanuzi zaidi unahitajika kuhusu kuwarejesha shuleni waliopata ujauzito

HIVI karibuni serikali ilitoa Waraka wa Elimu Namba 2 wa mwaka 2021 kuhusu urejeshwaji shuleni wa wanafunzi waliokatiza masomo katika elimu ya msingi na sekondari kwa sababu mbalimbali.

Wanafunzi wanaohusika ni waliokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali kama utoro, utovu wa nidhani na kupata ujauzito. Wengine ni walioshindwa kuhudhuria masomo kwa muda mrefu kutokana na matatizo ya kifamilia au wazazi kuhama maeneo bila kufuata taratibu za uhamisho wa watoto wao.

Aidha, utekelezaji wa waraka huo ambao ulianza Novemba 24, mwaka huu, umeangalia maeneo matano ambayo ni wanafunzi watakaokatiza masomo kutokana na ujauzito au utoro wataruhusiwa kurudi shuleni ndani ya miaka miwili tangu walipokatiza masomo.

Wakuu wa shule na walimu wakuu wametakiwa wahakikishe wanafunzi waliokatiza masomo na kurudi shuleni wanapata huduma za ushauri na unasihi ili kuwajenga kisaikolojia sambamba na wanafunzi wengine walioko shuleni.

Pia wakuu hao wa shule wametakiwa kuhakikisha mwanafunzi aliyekatiza masomo anarejea mwanzoni mwa mwaka wa masomo katika darasa alilokuwa anasoma. Aidha, walimu wahakikishe mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji unafanyika katika mazingira bora kwa wanafunzi wote.

Viongozi wa elimu katika ngazi zote wametakiwa wafuatilie na kutathmini utekelezaji wa waraka huo, huku mipaka ya waraka ikitajwa kuwa haitahusu wanafunzi waliofukuzwa shule kutokana na makosa yenye mwelekeo wa jinai au mwenendo unaohatarisha amani shuleni na kwamba watakaothibitika kutenda makosa hayo na kufukuzwa shule wanashauriwa kuendelea na masomo kupitia elimu nje ya mfumo rasmi. Uamuzi huu umepokewa kwa shangwe kubwa na watetezi wa haki za wasichana na watoto kwa kuwa wako ambao walipata ujauzito kwa kubakwa na si kwamba walijiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi wakiwa masomoni.

Ninaipongeza serikali kwa uamuzi huu kwa kuwa sasa unakwenda kuongeza idadi ya wasichana ambao ndoto zao zingekufa kwasababu ya ujauzito, lakini sasa tutakuwa na watu walioelimika watakaolea watoto wao vyema na kutoa mchango kwenye maendeleo ya familia zao na taifa kwa ujumla.

Wengi walijikuta wakikatisha ndoto zao na kushindwa kujiendeleza na matokeo yake kuendelea kupunguza idadi ya wasichana wasomi na wanawake wa baadaye ambao watatoa mchango kwa taifa lao.

Kwa upande mwingine, wako wanaosema uamuzi huo utawafanya wanafunzi wanaojihusisha na mapenzi kuwa ni jambo la kawaida kwa kuwa hakuna adhabu ya kuwafanya wasiendelee na masomo, bali baadaye watarudi na huenda itachochea ongezeko la mimba za ututoni.

Benki ya Dunia (WB) na mashirika mengine ya kimataifa yaliyo ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali yamepongeza uamuzi huo kwa kuwa sasa wasichana hao watatimiza ndoto zao na kuwa wasomi kama wengine.

WB imeeleza kuwa wanafunzi 120,000 huacha masomo kila mwaka kutokana na sababu mbalimbali na kati yao 6,500 ni wasichana na mama wadogo ambao wameshindwa kuendelea na masomo kwa sababu ya ujauzito.

Maswali yaliyopo kwa watu ni je, ndiyo ruksa mabinti wa umri mdogo kushiriki kwenye kujamiiana? Je, itakuwa kwa mimba moja na mtoto mmoja tu au anaweza kufululiza kupata ujauzito, kujifungua baada ya miaka miwili anarudi shule, mwakani anabeba mimba nyingine na nyingine? Pia ataruhusiwa kwenda na mwanawe shuleni na kama kuna vituo vya watoto wadogo shuleni?

Ni muhimu maswali haya yakajibiwa na serikali ili kurahisisha utekeleza wa waraka huu na kuwafanya wasome na kufikia malengo yao, ili shuleni pasigeuke kuwa mahali pa kuwaumiza tena kwa kuwahukumu kutokana na yaliyotokea nyuma katika maisha yao.

Lakini ni namna watoto hawa watarudi kwenye shule zile zile ambazo wenzao walijua kuwa walipata mimba. Lakini hawajui walipata kwa kukubali, kurubuniwa au kubakwa na huenda kutakuwa na unyanyapaa au kuwaumiza kisaikolojia kupitia lugha mbalimbali kuwa tayari wameshaondoka kwenye usichana na sasa ni mama. Natarajia kuona wanafunzi walioko shuleni wakielimishwa kwa nini ni muhimu wenzao wakarudi shuleni ili wawapokee na kuendelea kushirikiana nao kuliko kuwanyanyapaa na kuwaumiza kisaikolojia kupitia maneno.

Waraka umetaka walimu kutoa ushauri nasihi kwa wanafunzi hawa jambo ambalo ni muhimu sana ikiwa litatekelezwa kikamilifu ili kuwajengea ujasiri wa kukubali hali halisi na kurudi kwenye ndoto zao. Lakini ni muhimu jamii inayowazunguka nayo ikawa na uelewa wa kutosha utakaosaidia wanafunzi hao kusoma kama wengine na siyo kunyooshewa vidole.

Ni muhimu sana kukawa na utaratibu wa walimu waliojengewa uwezo wa kuwasaidia kisaikolojia wanafunzi kama hawa kuliko kuwaacha jumla, shule ziandae utaratibu kwa kuwa kwa tuliosoma shule za umma tunajua hakuna msaada wa kinasihi unaotolewa na hasa watoto wanapopitia changamoto mbalimbali kama za kubakwa, kulawitiwa, kunajisiwa au wanapokuwa katika hali ya hedhi matokeo yake wengi wanaacha shule kwa kuwa wananyooshewa vidole na wanafunzi wenzao.

Ninaamini waraka huu utatekelezwa ipasavyo, pia ni muhimu ukasambazwa kila mahali ili kuwe na uelewa kwa jamii na wazazi ili waruhusu watoto wao kuendelea na masomo. Lakini ni muhimu wazazi na jamii wakaendelea na jitihada za kuelimisha umma na wasichana juu ya umuhimu wa kujitunza na kuwaacha watoto wa kike watimize ndoto zao.

Pia ni muhimu kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji ili kuepusha usumbufu wowote, kuwe na shule za mfano ambazo zimeweza kuwapokea wanafunzi hawa wakaendelea na masomo bila usumbufu ikiwamo kufuatilia taaluma yao baada ya muda fulani ili kuonyesha wale waliofanya vizuri.











Novemba 13, mwaka huu ilikuwa siku ya kukumbukwa kwa familia ya Semkuya, baada ya mtoto wao Richard John kufunga ndoa na Ester Ezekiel katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Makubuli, kisha sherehe ya kuwapongeza ikafanyika katika ukumbi wa Vicktory uliopo Kimara Temboni jijini Dar es Salaam.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

# USOKOSE VIATU HIVI

UNAWEZA kuwa na viatu vingi kwenye kabati lako mpaka unasahau idadi yake na wakati mwingine unajiuliza kwa nini unamiliki idadi hiyo kubwa.

Watu wenye idadi kubwa ya viatu utakuta vimekaa tu kabatini, mpaka vinaharibika bila kuvaliwa.

Sasa ili kuepuka kurundika viatu usivyovivaa kabatini kwako, unatakiwa kufuata mtiririko huu.

Kama ilivyo kwenye mavazi, kwenye viatu pia kuna vile vya muhimu ambavyo hupaswi kukosa kuwa navyo.

Viatu ikiwamo Stilletto, hususani nyeusi ina uwezo wa kubadili mwonekano wowote ule, ni lazima kuwa navyo ndani ya nyumba yako.

Aina ya pili ni viatu vya wazi, ni kwaajili ya siku unazotaka kupumzisha miguu kama ni mtu wa kupenda kuvaa viatu virefu mara nyingi. Pia ni vizuri kwa safari fupi na kuna baadhi ya mavazi na shughuli ambazo huitaji viatu 'simple' vinavyokupa amani.

Mules aina yoyote

Aina ya tatu ni Mules, hivi viatu vinashika kasi kwa kupendwa. Aina hii ni vile vya kupachika mguu tu wakati wa kuvaa.

Vina raha na vinavutia, unaweza kuwa na mules fupi au zenye kisigino kirefu, ni uamuzi yako tu.

Aina ya nne ni viatu virefu 'High heel', vyenye kisigino kinene. Kuna siku unatamani kuvaa kiatu kirefu lakini hutaki zile stress za kubalance kiatu na maumivu.

Kiatu kirefu chenye kisigino kinene uwa rahisi zaidi kutembelea maana kimpa mtu usalama wa kutosha.

Raba ni aina ya viatu unapaswa kuwa navyo kutokana na kuwa na mwonekano wa kawaida, lakini bado kitakupa matokeo mazuri utakapovaa.

Viatu vya aina ya Boots, vina raha yake pale unapovaa hasa kutokana na mtindo wake. Unaweza kununua mitindo mbalimbali ili kukupa chaguo zuri linaloendana na nguo zako.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# KICHEKO MURUA

# Meno meupee yanayong'ara

MENO pamoja na kuwa zana muhimu katika kumeng'enya chakula, lakini kwa upande mwingine ni sehemu ya pambo kwa mwanamke.

Wanawake wenye meno meupe na yanayong'aa wana mvuto zaidi kutokana na mwonekano wao wenye kujiamini na tabasamu zuri.

Katika kitu ambacho wengi hawafahamu ni kwamba, kama unafahamu mbinu sahihi ya kusafisha meno, basi kicheko kwako kitakuwa jambo la kawaida kutokana na meno kuwa masafi na yanayong'aa.

Leo tutaelekezana jinsi ya kusafisha meno ili kuondoa rangi ya njano kutokana na vyakula pamoja na vinywaji tunavyotumia kila siku.

BAKING SODA NA JUISI YA NDIMU

Baking soda ina Sodium Bicarbonate ambayo inasaidia kuondoa madoa na rangi ukichanganya na ile juisi ya ndimu inasaidia kupunguza alkaline iliyopo kwenye ndimu.

Changanya juisi ya ndimu pamoja na baking soda kupata mchanganyiko mzito.

Futa meno kuondoa mate kisha chukua mswaki wako, chota mchanganyiko kisha paka kwenye meno (usipige nayo mswaki kama unavyotumia dawa ya mswaki, paka tu).

Iache kwa dakika moja kisha sukutua na maji, fanya hivyo mara moja kwa wiki.

**TUMIA MAFUTA YA NAZI**

Tumia mafuta ya nazi kila asubuhi kusukutua kabla hujapiga mswaki.

Weka kiasi cha kutosha mdomoni kisha anza kusukutua, zungusha katika kila kona, fanya kama unavuta na kuyasukuma humo mdomoni lakini usiyameze.

Fanya hivi kwa dakika 10-15. Ukishamaliza hivyo sukutua kisha piga mswaki kama kawaida, dawa hizi zina uwezo wa kulinda meno na wadudu na kuyatakatisha.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# JIPE RAHA NA UBUYU

UBUYU wa Zanzibar umekuwa maarufu kutokana na kuwa na ladha tamu na harufu inayovutia.

Watu wengi wanachangamkia kula ubuyu wa Zanzibar, lakini kama ukishindwa kununua kwa wingi na kukidhi hamu yako, basi unaweza kupika nyumbani na ukafurahia maisha.

Katika safu yetu ya mapishi, hizi ni baadhi ya mbunu za namna ya kuupika ubuyu huu mtamu.

**Mahitaji**

Sukari vikombe viwili, maji vikombe viwili, unga wa ubuyu kikombe, ubuyu vikombe vinne, robo kijiko cha pilipili ya unga, robo kijiko cha chumvi, robo kijiko cha hiliki ya unga na rangi nyekundu au yeyote utakavyopenda.

**JINSI YA KUPIKA**

Chukua sufuria weka maji, sukari, chumvi na pilpili ya unga, rangi nahiliki. Moto uwe juu kiasi na changanya vyote hivyo vipike vizuri.

Wakati viungo vinaanza kuchemka utakuta rojo ya mapovu, endelea kukoroga ili rojo iive vizuri.

Uji wa viungo unapokuwa mzito, hapo chota kidogo katika mwiko na weka kidole ili kujua kama uji wako unanata au la. Uji unatakiwa unate na ndio utakuwa tayari.

Kisha mimina tunda za ubuyu, halafu changanya vizuri katika uji wa viungo.

Ukishachanganya tunda na uji wa viungo, acha uchemke kwa dakika kama 10, kisha mimina unga wa ubuyu na changanya vizuri tena.

Endelea kuchemsha mpaka unaona sukari inaanza kuganda na kung'aa na kushika vizuri kwenye ubuyu.

Hapo sasa ubuyu wako utakuwa tayari, mimina kwenye chombo kinachoingiza hewa ili ukauke vizuri.

Unaweza kula ubuyu wako wakati wowote kama kiburudisho.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Dondoo za usafi wa bafu na choo

USAFI wa nyumba wa mara kwa mara ni nguzo kubwa ya kuistawisha na kuipendezesha kwa kiwango kikubwa.

Nyumba isipofanyiwa usafi wa mara kwa mara huchakaa mapema na hata kuharibika kabisa. Usafi wa nyumba ninaozungumzia ni wa sehemu zote za nyumba na si katika eneo la sebule, chumba cha kulala au cha kupikia tu.

Nafahamu kwamba huenda kila mtu ana mbinu yake ya kusafisha nyumba yake lakini leo nitapenda kukuongezea baadhi ya dondoo nyingine za namna ya kusafisha nyumba yako hususani katika sehemu ya bafu na choo.

Nataka tujifunze namna ya kusafisha kuta katika sehemu hiyo ya bafu, sinki, bomba, eneo la kuogea na bakuli la choo.

Kabla ya kuanza kusafisha bafuni, kwanza ondoa vitu vyote vya kuhamishika kama vile vizulia, tenga la nguo chafu, meza au kabati na ndoo ya taka, huku ukihakikisha dirisha linakuwa safi.

Baada ya hapo unaweza kuondoa buibui kwenye kona za dari ikifuatiwa na kufuta vumbi mlango katika sehemu ya ndani na nje.

Kwa ujumla, wakati wa kusafisha ni vyema kuanzia juu na kushuka chini ili kuruhusu taka za vumbi na buibui zimwagike sakafuni kwa ajili ya kusafisha mwishoni na unapaswa kutumia kitambaa kufutia au fagio.

Unaweza kumiminia sabuni za kusafishia kwenye bakuli la choo na kuiacha kwa dakika kadhaa ili uchafu ulainike. Baada ya hapo unaweza pia kuweka dawa ya unga wa kusafishia katika sehemu zenye uchafu ili iwe rahisi wakati unasugua.

Ni vyema ukazingatia maelezo ya dawa ya kusafishia ili kuwa na uhakika unatumia kiasi sahihi ambacho hakiwezi kuharibu.

Katika kuta za bafu pia unapaswa kupaka sabuni au dawa zingine za kusafishia endapo zitakuwa za marumaru na kwa kutumia sponji au brashi, unaweza kusugua sehemu uliyoweka sabuni hiyo huku ukihakikisha unaisuuza kuondoa michirizi yote michafu. Kama ukuta ni wa karibu na sinki au bakuli la choo, ukaushe kwa taulo.

Ni muhimu kukumbuka kuvaa glovu wakati wa kusugua kwani baadhi ya dawa na sabuni zinaweza kuchubua ngozi.

Pia mswaki wa zamani usiotumika unaweza kutumika kuondoa uchafu kutoka eneo la kati ya bomba na mishikio yake na unapaswa kuepuka kutumia blashi la kusugulia bakuli la choo, kusugulia sinki kwa sababu unaweza kusambaza maradhi.

Safisha kioo kwa kutumia ama maji na taulo au dawa ya kusafishia vioo na taulo. Safisha nje ya choo ukianza na ile sehemu ya juu ya kuvuta maji, kwa taratibu unaweza kuendelea kusafisha eneo lote la nje ya choo ambalo ni pamoja na mfuniko na eneo la chini ya sehemu ya kukalia na kupafuta na taulo.

Kwa upande wa sakafu, hakikisha usafi wako unaanzia sehemu zilizojificha hadi zile za wazi na ni vyema kusafisha vumbi na uchafu wote ulio chini eneo la choo lilipounganika na sakafu.

Subiri kidogo sakafu ikauke ndipo urudishe vile vitu ulivyoondoa awali.

Ili kuweka bafu lako katika hali ya usafi na kupunguza kutumia nguvu kubwa ya kusafisha, unatakiwa uwe unasafisha maeneo mbalimbali ya bafu baada ya kuyatumia.

Ni vyema kusafisha bakuli la choo kila baada ya kulitumia, eneo la sinki pamoja na eneo la kuogea hata kama sehemu hizo hazionekani kuchafuka.



## Tumia sehemu ya chini ya ngazi kubuni vitu mbalimbali




Dondoo za kuchagua stendi za kuwekea nguo

BAADHI ya watu hawapendi nguo zao kuzihifadhi ndani ya makabati kwa kuhofia kujikunja, badala yake wanatumia stendi maalum za kuhifadhia nguo ambazo ni rahisi kutumia na haichukui nafasi kubwa. Kutokana na umuhimu wake zifuatazo ni dondoo za kuchagua stendi nzuri ya kuning'iniza nguo chumbani kwako.

1: Chagua stendi iliyotengenezwa na chuma laini kiasi ili kukupa urahisi wa kuhamisha kutoka sehemu moja hadi nyingine.
2: Angalia ukubwa na uimara wa stendi kabla ya kuinunua. Vitu hivyo ni muhimu kuviangalia ili stendi yako ilingane na nafasi ya chumba chako na iweze kudumu kwa muda mrefu.
3: Chagua stendi yenye umbo zuri, kwani pamoja na kuwa nyezo ya kuhifadhia nguo pia ni sehemu ya mapambo ndani ya chuma na hivyo angalia yenye kuvutia zaidi.
4: Hakikisha stendi inakuwa na rangi inayoendana na chumba chako, kwa wale wanaopenda rangi za kuiva wanashauriwa kuwa makini kwani aina hizo za rangi mara nyingi hazipendezi kuwa ndani.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

HATA UKINUNA MAISHA YANASONGA

HABARI KIMATAIFA

# Algeria yafanya uchaguzi bila Bouteffika

**ALGIERS,** ALGERIA

RAIA wa Algeria jana walipiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa ambao utaonyesha uwezo wa Rais Abdelmadjid Tebboune, wa kuifuta enzi ya utawala wa miongo miwili ya kiongozi aliyemtangulia hayati Abdelaziz Bouteflika.

Tume ya uchaguzi ilisema zaidi ya wagombea 15,000 walishiriki uchaguzi huo wa kujaza nafasi za viongozi wa halmashauri za miji, majiji na majimbo katika taifa hilo la Afrika Kaskazini.

Hata hivyo licha ya kampeni kubwa wafuatiliaji wa uchaguzi huo wametabiri kutakuwa na idadi ndogo ya wapiga kura kama ilivyoshuhudiwa katika chaguzi zilizotangulia tangu kuangushwa kwa utawala wa Bouteflika Aprili, mwaka 2019. Uchaguzi huo utakuwa wa tatu kwa ngazi ya kitaifa chini ya Rais Tebboune, ambaye ameapa kuzifanyia mageuzi mapana taasisi za dola alizorithi kutoka kwa Bouteflika, aliyefariki mwezi Septemba, mwaka huu.

**DW**

# Utulivu warejea visiwa vya Solomon

**HONIARA,** SOLOMON

HALI ya utulivu imerejea kwenye mji mkuu wa visiwa vya Solomon, Honiara baada ya siku kadhaa za machafuko yaliyosababisha vifo vya watu watatu na uharibifu mkubwa wa mali.

Vituo vya mafuta, maduka na biashara nyingine zimeanza kufunguliwa tena na wakazi wa mji huo wameanza kununua mahitaji muhimu baada ya kupungua kwa vurugu hizo.

Kwa siku tatu mfululizo makundi ya watu wenye hasira yalifanya vurugu mjini Honiara kushikiza kujiuzulu kwa Waziri Mkuu, Manasseh Sogavare.

Hasira hizo imechochewa na kudorora kwa hali ya uchumi, ukosefu wa ajira na kuongezeka kwa umasikini kwenye visiwa hivyo vya bahari ya Pasifiki.

**DW**

# Kirusi Omicron chazidi kuleta hofu duniani

**GENEVA,** USWISI

SHIRIKA la afya duniani (WHO) limetangaza jina la kirusi kipya cha corona kuwa Omicron na kukitaja kama kirusi kinachotia hofu.

Kirusi hicho kinaelezwa kuwa kina orodha ndefu ya mabadiliko ya kimaumbile na tayari ushahidi unaonyesha kuongezeka kwa hatari ya ongezeko la maambukizi.

Kwa mara ya kwanza aina hiyo ya kirusi kiliripotiwa kugundulika nchini Afrika Kusini, Novemba 24, mwaka huu na imebainika kusambaa katika mataifa ya Botswana, Ubelgiji, Hong Kong na Israeli.

Nchi kadhaa duniani sasa zimeamua kuweka masharti ya usafiri wa kutoka au kuelekea Afrika Kusini.

Wasafiri kutoka Afrika Kusini, Namibia, Zimbabwe, Lesotho na Eswatini hawataweza kuingia nchini Uingereza isipokuwa kama watakuwa ni raia wa Uingereza na Ireland au wakazi wa Uingereza.

Maofisa wa Marekani walisema kuwa safari za kutoka Afrika Kusini, Botswana, Zimbabwe, Namibia, Lesotho, Eswatini, Msumbiji na Malawi zitazuiwa.

WHO ilisema idadi ya visa vya aina mpya ya virusi vya corona, ambavyo awali vilipewa jina la B.1.1.529, inaonekana kuongezeka katika karibu majimbo yote ya Afrika Kusini.

"Aina hii ina orodha ndefu ya mabadiliko, ambayo baadhi yake ni ya kuhofia," lilisema shirika hilo.

Hata hivyo, WHO ilisema itachukua wiki kadhaa kuelewa athari za kirusi hicho kipya, huku wanasayansi wakifanya juhudi za kubaini ni kwa jinsi gani kinasambaa. Ofisa wa ngazi ya juu wa Uingereza alionya kuwa chanjo huenda zisiwe na ufanisi dhidi ya aina mpya ya virusi vya corona.

Lakini Profesa James Naismith, mwanabaiolojia wa maumbile kutoka Chuo kikuu cha Oxford, alisema hiyo ni habari mbaya lakini sio mwisho wa dunia.

Alisema mabadiliko ya muundo au maumbile katika aina mpya ya kirusi yanaonyesha kuwa kinaweza kusambaa haraka zaidi, lakini usambaaji wake sio rahisi kama inavyosambaa amino acid .

Nchini Afrika Kusini ni asilimia 24 pekee ya watu waliopata chanjo kamili, jambo linaloweza kuchochea ongezeko la haraka la visa.

Wakati huo huo, Mkuu wa masuala ya magonjwa ya maambukizi nchini Marekani Dkt Anthony Fauci alisema kuwa huku ripoti kuhusu aina mpya ya kirusi zikiashiria hatari, kuna uwezekano bado chanjo inaweza kuzuia kuugua.

WHO ilionya nchi kuweka masharti ya kusafiri, ikisema zinapaswa kuangalia zaidi udhibiti wa maambukizi kwa kuzingatia mbinu za kisayansi na hatari yake.

**BBC**



Baadhi ya wasafiri wakiwa katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Oliver Tambo, jijini Johannesburg, wakisubiri ndege baada ya mataifa mbalimbali kupiga marufuku safari za kwenda nchini humo kutokana na hofu ya virusi vipya vya korona. **(PICHA: Associated Press)**

# Marekani yaonya mgogoro wa Ethiopia

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI wa Mambo ya kigeni wa Marekani, Antony Blinken, amesema ana wasiwasi na kuongezeka kwa mapigano ya kijeshi kwenye mzozo nchini Ethiopia. Blinken, alitoa wito wa kufanyika haraka kwa mazungumzo ya pande mbili kwa ajili ya kukomesha mapigano.

Hayo yameelezwa kwenye taarifa iliyotolewa na msemaji wa wizara hiyo, ikimnukuu waziri Blinken aliyekuwa na mazungumzo na Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya kuhusu mzozo wa Ethiopia. Matamshi ya Blinken yalitolewa saa chache baada ya Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, kuonekana kupitia televisheni ya taifa akiwa mstari wa mbele pamoja na wanajeshi kwenye uwanja wa mapambano.

Zaidi ya mwaka mmoja serikali inapigana kuwadhibiti wapiganaji wa jimbo la Kaskazini la Tigray katika mzozo ambao umesababisha vifo vya maelfu ya watu na kuwalazimisha wengine kuhama makazi yao.

**BBC**

MAKALA

# UTARATIBU WA CHAKULA SHULENI UTAZAMWE UPYA



Na Magabilo Masambu

SERIKALI ya awamu ya tano chini ya Rais Hayati John Magufuli, ilipitisha Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2015 kuhusu utekelezaji wa elimu bila malipo kwa shule za sekondari. Waraka huo ulioanza kutekelezwa Januari, 2016 ulifuta nyaraka kadhaa zilizokuwa zikitoa maelekezo ya michango kwa shule za sekondari.

Miongoni mwa nyaraka zilizofutwa ni Waraka Na. 9 wa mwaka 1998 ulioelekeza tozo ya ada ya Sh. 40,000 kwa wanafunzi wa shule za kutwa na Sh. 70,000 kwa shule za bweni na Waraka Namba 11 wa mwaka 2004 uliopunguza ada kwa wanafunzi wa kutwa kutoka Sh. 40,000 mpaka 20,000.

Nyingine ni Waraka Namba 8 wa mwaka 2011 uliotoa maelekezo ya michango mbalimbali kupitia kamati au bodi za shule, Waraka Namba 1 wa mwaka 2012 kuhusu kurejesha ada za mitihani kwa shule za sekondari za serikali na Waraka Namba 1 wa mwaka 2013 kuhusu uchangiaji wa gharama za ukaguzi wa shule.

Waraka huu pia ulitoa maelekezo kuhusu majukumu ya wazazi kama kuwanunulia watoto wao mahitaji ya msingi kama sare za shule, vifaa vya kujifunzia kama madaftari na kalamu. Pia ulielekeza kuhusu suala la chakula kwa watoto wawapo shuleni kwamba linawahusu wazazi.

Bahati mbaya wakati suala la elimu bila malipo linaanza, palikuwapo na matamko mbalimbali ya wanasiasa yaliyoonyesha kwamba elimu ni bure kwelikweli kwa maana kwamba mzazi hakutakiwa kushiriki au kuchangia kwa chochote. Matamko hayo yalisababisha baadhi ya wazazi wakayabeba matamko hayo kiasi cha kufanya hata suala la chakula waone kama ni jukumu la serikali.

Ukweli ni kwamba hali ya watoto katika shule zetu kuhusu ulaji wao ni mbaya sana. Kuna hatari ya kuwasababishia matatizo ya muda mrefu yatakayotokana na lishe duni au kutokula kabisa wawapo shuleni. Katika shule za kutwa, wanafunzi wengi hawalipiwi chakula na wazazi wao jambo ambalo ni hatari sana kwa afya zao za sasa na baadaye.

Ni ukweli vilevile kuwa serikali kwa upande wake imejitahidi angalau kuondoa ada ambazo zilionekana kama kikwazo kwa wanafunzi wengi kuendelea na masomo, hivyo kufanya hata uandikishwaji wa wanafunzi kuongezeka madarufu lakini je suala la chakula nani analifikiria?

Je, tunafahamu kwamba watoto walio wengi wanashinda njaa wawapo shuleni? Matatizo yatakayotokana na kutopata chakula kama vidonda vya tumbo vya kudumu, magonjwa mengine na ukosefu wa vitamini nani alaumiwe je ni serikali, mzazi au shule? Nani wa kulisimamia hili ili watoto wasiadhibiwe bila makosa?

Ukweli kwamba sasa ni dhahili tumekazania matokeo makubwa haupingiki, lakini matokeo makubwa kwa watoto watakaokuwa wanaugua leo na kesho wakiwa watu wazima yana maana gani? Kwa kweli haiingii akilini mtoto anasoma miaka minne toka kidato cha kwanza mpaka cha nne kila siku mchana hapati chakula na wakati mwingine akirudi nyumbani pia jioni ama analala njaa au anapata bora chakula.

Zamani shule zote za kutwa muda wa kutoka ilikuwa saa 8:00 mchana maana yake tulipata chakula cha mchana nyumbani. Leo shule za kutwa wanafunzi wanatoka saa 11:00 au 12:00 jioni kwa hoja kwamba wanakula shule lakini kikubwa ikiwa hofu ya matokeo makubwa kwamba wakiachiwa mchana hawatasoma.

Baadhi ya shule, hasa za binafsi, wameanzisha utamaduni hata wa kuwalazimisha watoto wadogo kuamka asubuhi sana kuingia darasani au kuwabakiza jioni baada ya masomo lengo matokeo makubwa sasa. Je, tumepima madhara yatakayotokana na taratibu hizi au kazi yetu ni kuangalia matokeo tu? Kuna haja gani ya kuwa na matokeo makubwa yenye athari za kiafya kwa watoto wetu? Si ni bora wapate matokeo ya kawaida lakini wawe na afya bora?

Ili kuwa na taifa imara, lazima tutengeneze kizazi chenye afya bora, watu watakaokuwa wanafikiri na kutenda vizuri, hakuna haja ya kuwa na matokeo mazuri kwenye cheti, lakini hutaweza kufanya kazi kwa ufanisi kutokana magonjwa uliyoyatengeneza kwa kukosa chakura bora.

Tutakubaliana kwamba pamoja na uzima kutoka kwa Mungu, chakula bora hupunguza uwezekano wa vifo vinavyosababishwa na magonjwa yanayotokana na lishe mbovu. Anayekula ugali wenye mchanganyiko wa unga wa mhogo na dona hawezi kufanana na anayekula vyakula vya kukoboa. Anayekula kande kila siku hatafanana na anayebadili chakula pamoja na matunda na kadhalika.

Ushauri wangu ni kwamba kama tunaona suala la chakula shuleni limeshindikana, utaratibu wa zamani wa kutoka saa 8:00 mchana urudishwe, ili kila mtoto akale nyumbani kwao badala ya kuwaumiza. Pili, inawezekana wazazi hawana pesa lakini wana mahindi, maharagwe na mchele, hivyo ni vyema na haki wakubaliane na kamati za shule wachange vyakula na pesa kidogo za wapishi.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Msondo ilivyozuia Tx Moshi, Nico kuhama



Na Adam Fungamwango

BENDI ya Msondo Ngoma ndiyo kwa kiasi kikubwa inayoongoza kwa kuondokewa na wanamuziki wengi kuliko bendi yoyote ile nchini Tanzania.

Tangu wakati inaitwa NUTA Jazz, baadaye ikaja Juwata Jazz, halafu ikaitwa OTTU Jazz, mpaka ikawa Msondo Ngoma Music Band, imepitiwa na wanamuziki wengi mahiri kabisa, lakini wengi wao pia wakahama.

Hata hivyo, Msondo iliwapokea baadhi ya wanamuziki ambao waliihama bendi hiyo, wakaja kufariki wakiwa kwenye bendi hiyo. Ni kama baba tu aliyewaacha watoto wake waende wakatafute ughaibuni, halafu baadaye wanarejea na walichokitafuta na umauti unawakuta wakiwa nyumbani kwenye bendi mama.

Baadhi yao ni kama Muhidini Mwalimu Gurumo, Athumani Momba, Suleiman Mbwembwe, Shaaban Dede na wengine ambao kwa nyakati tofauti waliihama Msondo na kusababisha tafrani kubwa. Lakini baada ya miaka mingi kupita walirejea nyumbani, wakapokelewa na bahati mbaya umauti ukawakuta wakiwa kwenye bendi hiyo.

Pamoja na kwamba Msondo imekuwa ikipokea wanamuziki wengi na baadaye wanahama, kuna baadhi ya wanamuziki ambao mashabiki wenyewe wa bendi hawakutaka wahame. Ukiona mwanamuziki wa bendi hiyo amehama pamoja na kwamba baadhi walipata misukosuko, mashabiki hawakuona sana umuhimu wao pamoja na kwamba mapengo yalionekana kwa muda.

Hakuna yeyote asiyewajua mashabiki wa bendi ya Msondo. Ni mashabiki ambao kwanza wanaipenda sana bendi yao kuliko kitu kingine chochote. Wako tayari kufanya chochote, kujitolea kwa hali na mali kwa manufaa na ustawi wa bendi hiyo.

Kuna wanamuziki wawili kwenye historia ya bendi hiyo ambao hawakuhama hadi wamefia Msondo, ingawa kulikuwa na majaribio kadhaa ya kutaka kunyakuliwa na bendi zingine.

Wao wenyewe, pamoja na nguvu za mashabiki zilitumika kuwabakisha. Ni umauti tu ndiyo uliowatenganisha wanamuziki hao na Msondo na si binadamu. Hao ni Ni Tx Moshi William na Nico Zengekala. Hawa wote walikuwa waimbaji na watunzi ambao waliondokea kuwa vipenzi vya mashabiki wa bendi hiyo.

Tx Moshi alijiunga na Msondo mwaka 1982 akitokea Polisi Jazz Band na alifariki dunia mwaka 2006, huku Nico Zengekala, raia wa Kenya, kule Taita, Voi, akijiunga na bendi hiyo mwaka 1985 hadi kifo kilipomchukua mwaka 1987. Huyu alitokea bendi ya Les Cubano ya Morogoro. Alikuwa mwimbaji kijana kabisa aliyefariki dunia akiwa hajazidi umri wa miaka 25, lakini alikuwa mlemavu na macho.

Aliletwa nchini na baadhi ya wanamuziki wa bendi ya Super Volcano ya Mbaraka Mwinshehe, ambaye baada ya kufia nchini Kenya, aliacha wanamuziki huko wakiendelea kujitafutia maisha. Baadaye waliamua kurejea nyumbani kwenye mkoa wao wa Morogoro na kuunda bendi, huku wakimchukua Nico na kuvuka naye mipaka.

Alidumu muda mfupi tu na kujiunga na Msondo kutokana na uwezo mkubwa wa kimuziki na sauti yake tamu. Jaribio la kwanza lilikuwa ni DDC Mlimani Park kama kawaida yao kuchukua wanamuziki wa Msondo, lakini kwa Moshi walichemka.

Kwa maelezo yake mwenyewe Moshi kabla hajafariki dunia, wakati akiwa amefichwa na anataka kutambulishwa na Sikinde DDC Kariakoo, baadhi ya mashabiki wa Msondo walimfuata wakiwa na bastola mkononi, wakampora mbele ya watu wa Sikinde na kumpeleka DDC Keko ambako Msondo ilikuwa inapiga. Alisema hakujua walipata taarifa wapi na walikujaje kwani wakati huo hakukuwa na simu.

Baada ya kifo cha George Peter Kinyonga, mwanamuziki ambaye ndiye aliyemfanya Moshi kupenda muziki na kuiga sauti yake, kaka yake Wilson Peter alitaka kumchukua ili kwenda kuziba pengo lake, lakini mashabiki wa Msondo walikataa, wakampiga mkwara na kuweka walinzi sehemu zote, Uwanja wa Ndege, kwenye vituo vya mabasi na Bandari zote kuwa Moshi akionekana basi azuiwe na kuna watu watakuja kumchukua. Ikashindikana.

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, TOT Plus nao ilikuwa nusura wamchukue, kwa kumpa pesa, gari, lakini baadhi ya mashabiki wa Msondo waliingilia kati dili hilo kwa kumrudishia pesa Kapteni John Komba (sasa marehemu). Gari likarudishwa pia huku wao wakimpeleka 'show room' kuchagua gari analolipenda, ili mradi tu abaki Msondo.

Kwa upande wa Nico kwanza aliibwa na kupelekwa Tancut Almasi ya mwanzo kabisa, Isaya Swahiba, ambaye ni rafiki yake aliyekuwa anamshika mkono ndiye aliyekula dili hilo, bila Zengekala kujua.

Wakati Nico akidhania bado yupo Msondo, aliambiwa hapa ni Iringa na hii ni Tancut Alamsi bendi mpya. Nico alikasirika, akagoma kula kwa siku tatu, wakaamua kuachana naye, akarudishwa Msondo. Wakati huo magazeti yalishaandika 'Nico atoweka Msondo'.

Fitna kwa wapinzani wa Msondo ikatembea, akatekwa kwa mara ya pili na kurudishwa kwao Kenya. Alikaa kwa muda wa mwezi mmoja, akatafuta nauli mwenyewe, tena ya ndege, akarejea Msondo.

Jaribio la tatu ni Orchestra Safari Sound wana Ndekule. Nico alipenda kwenda kwenye bendi hiyo kuimba nyimbo za Bitchuka hasa alioupenda ni 'Sosy'. Alifanya hivyo wakati Msondo haifanyi maonyesho hasa nyakati za mfungo wa Ramadhani.

Kukawa na tetesi au mpango wa kutaka kumchukua moja kwa moja. Mashabiki wa Msondo walipokisikia walipiga mkwara kuwa OSS ikimchukua Nico, basi labda akapige muziki nchini Kenya na si hapa Tanzania. Mpango huo ukafa.

Alifariki dunia Desemba 17 mtaa wa Sikukuu, Kariakoo, Dar es Salaam na kuzikwa kwao Mwatate, Voi, Taita, Mombasa, nchini Kenya.

# HADITHI

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

# Ajenda ya Siri-6

**Na Adam Fungamwangwo**
**(0716 350534)**

HAPANA, ni lazima niwasiliane na bosi wangu, Mkuu wa Idara wa Usalama, na aandike barua ya kukubali ninachotaka kufanya na hicho kinakuwa kuruhusu kwenda popote, kumfuata yeyote, kumhoji mtu yeyote, kuingia sehemu yoyote ile na wakati mwingine kufanya chochote, ikiwemo hata kujeruhi au kuua kama ikihitajika au kushindikana kwa hali ya kawaida."

"Sawa, mimi sikupingi kwa hilo."

"Kama watakuwa ni wafanyabiashara wenzake kwa sababu ya kudhulumiana, basi ninachotaka wajulikane ili nao wapelekwe mahakamani wakapate stahiki. Wakati Tina ananyongwa, basi na wao wakamatwe wapate adhabu inayowafaa. Na kama si wafanyabiashara, ila kuna mtu amemtuma tu kwa sababu zake au kikundi chochote kwa sababu zao tu, basi sitokubali kabisa kiwe uraiani. Nitawatafuta popote pale, ikwezekana hata kuingia chini ya ardhi, ili wapatikane. Kuanzia wiki ijayo naianza kazi hiyo."

"Hakuna tatizo, nakutakia kazi njema, ila kama kuna kitu utakuwa unahitaji cha kisheria zaidi, basi asisite kunipigia, njoo ofisini au niite kama kawaida tu."


"Hilo halina shaka." Eddy alijibu. Tinga alinyanyuka na kupeana mikono tena kama walivyofanya wakati alipowasili."

********************************

Gari aina ya Nissan Ariya la rangi nyeusi lilisimama karibu na kiwanja cha kuchezea mpira cha watoto maeneo ya Tegeta kwa Ndevu. Ilikuwa karibu kabisa na kituo cha mabasi. Ilikuwa majira ya saa 10:00 jioni. Kila mmoja alikuwa kwenye pilikapilika zake. Alishuka mtu mmoja mrefu kidogo, maji ya kunde, mwembamba, lakini mwenye mwili uliojengeka kimazoezi.

Alikuwa amevaa jeans iliyopauka na kukatwakatwa kama vijana wengine wa mjini. Alivaa fulana ya mikono mirefu iliyombana, yenye rangi ya zambarau. Alivaa pia miwani ya macho.

Hakuvaa hivyo kwa bahati mbaya. Hakutaka kuwa kivutio sana kwenye macho ya watu. Alikwenda moja kwa moja mpaka kwenye duka la dawa lililokuwa jirani. Juu ya mlango alikutana na maandishi ya 'Ni Sisi Pharmacy'. Aliusukuma na kuingia. Aliwakuta wateja watatu wakiwa wanahudumiwa. Hakutaka kuwabugudhi. Kwanza alionekana kama anataka huduma, lakini akawaacha kwanza wenzake wahudumiwe.




**"Hakuna tatizo, nakutakia kazi njema, ila kama kuna kitu utakuwa unahitaji cha kisheria zaidi, basi asisite kunipigia, njoo ofisini au niite kama kawaida tu." "Hilo halina shaka." Eddy alijibu. Tinga alinyanyuka na kupeana mikono tena kama walivyofanya wakati alipowasili."**

"Enhee nikusaidie nini kaka?" Ilikuwa sauti ya mwanamke aliyekuwa anauza ikimzindua. Macho yake alikuwa anaangalia vitu tofauti ndani humo.

"Samahani, nadhani mimi nachohitaji ni tofauti kidogo na hawa waliopita."

Jibu hilo lilionekana kumshangaza kidogo muuzaji huyo anayeonekana kabisa kukaribia miaka 30. Mshangao ulijionyesha wazi machoni mwake. "We kwani unahitaji nini?"

"Namuulizia Mwahija."

"Unamjua, au umeshawahi kumuona?"

"Hapana, ila kuna mtu amenielekeza nije kwake." "Mwahijaaa." Aliita.

Ndipo Eddy Kamal alipogundua kuwa aliyekuwa akizungumza naye si Mwahija kama ambavyo alikuwa anafikiri.

"Mbele ya duka hilo la dawa, kuna mlango mdogo ambao hawezi kuujua mpaka mtu akifungua. Nao pia umepangwa dawa mbalimbali na kuonekana kama ukuta.

Yoyote atakayefungua, ndipo anayeangalia atajua kuwa ulikuwa mlango wa mbao, uliotengenezwa kiufundi na kuonekana nao pia kama shefu ya kuwekea dawa. "Bibi, mgeni wako huyu."

Macho ya Eddy sasa yalikuwa yakimtazama msichana mmoja mrembo, ambaye hazidi miaka 25. Alikuwa amesuka nywele zake kwa mtindo wa yeboyebo ambao ulimfanya apendeze. Macho yake maangavu na rangi yake ya mwili, nguo alizovaa, vilimfanya aonekane msichana mrembo mbele ya warembo wenzake.

Alionekana kumshangaa mgeni asiyemtegemea na kumfahamu pia.

Eddy alitabasamu kwa nia ya kumwondoa hofu Mwahija. "Wewe ndiye Mwahija?"

Alishusha pumzi na kujibu "Wewe nani kakwambia mimi naitwa Mwahija?" Aliuliza kwa namna ya kejeli hivi.

Eddy alitabasamu tena. "Msichana mrembo kama wewe halafu jina lako liwe siri kama nyumba ya kuuza gongo kweli?"

"Enhee, unasemaje?" Bado Mwahija aliendelea kuuliza maswali na kuonekana kutoridhika kabisa na ujio wa mgeni huyo asiyemfahamu.

Kama kawaida, Eddy ni mzoefu mno kwa mambo hayo. Kwake haikuwa kitu kipya na cha ajabu, alichofanya safari hii alicheka. Lakini kicheko kifupi mno.

"Sikufikiri mrembo mzuri kama wewe unaweza kuwakaribisha wageni vibaya hivyo. Kama ni hivyo ngoja tu niondoke Mwahija Chota."

Mwahija alionekana kushtuka. Hata ule usimamaji wake wa nyodo na utazamaji wake kwa mgeni aliacha. Hakutegemea mgeni yule kufahamu jina la ukoo wake wa Chota.

Mara nyingi vijana wa kawaida wanaomfahamu jina wanamfahamu kwa jina la Mwahija. Na kama ikihitajika zaidi na hutumia jina la Mwahija Said. Ni sehemu chache sana na muhimu hutumia jina la ukoo Chota.

Kitendo cha mgeni yule kutaja jina la Chota kilimshtua na kuona hakuwa ni wa kawaida na kulikuwa na namna. Ama anatoka kijijini kwao au anawaifahamu familia yake, ndugu na wazazi, au vyovyote vinavyofanana na hivyo.

"Kwani wewe ni nani na umetoka wapi kaka?" Mwahija aliuliza kwa sauti tofauti na ile ya awali. Yeyote aliyekuwa akiwasikiliza bila kuwaona, angeweza kudhani ni watu wawili tofauti. Sasa aliuliza kwa adabu na heshima. Aliogopa kuwa mtu huyo huenda ni wa karibu familia yao au anamfahamu vizuri bila yeye kujua, hivyo sifa mbaya huenda zikafika kwao.

"Mimi naitwa Danny, nimekuja kwako, kuna mambo fulani naomba tuongee. Siyo marefu, ni ya kawaida tu, nilihitaji kupata ufafanuzi."

Bado Mwahija alikuwa kwenye mawazo. Hakujua mtu yule ni nani na alitaka nini. "Sasa tuongee hapa au wapi?"

"Ni wewe tu unapotaka, siwezi kukupangia dada yangu."

"Njoo huku ndani basi." Mwahija aliamua kumpekeka mgeni kwenye ofisi yao ambako hakukuwa na mtu yeyote kwa kuhofia huenda jambo lenyewe linaweza likawa la siri ambayo inamhusu kwa kuwa alikuwa ameshaanza kushuku huenda ni mambo ya nyumbani kwao Tanga.

Eddy aliingia na kuelekezwa kwenye kiti alichoambiwa akae.

"Kakusuka nani hizi nywele?" Eddy alianza mzaha wake kwa makusudi. Nia ilikuwa kumwondoa msichana huyo kwenye mawazo, kiburi, nyodo na hofu aliyokuwa nayo. Kwa mara ya kwanza Eddy alishuhudia Mwahija akitabasamu. Tabasamu lake lilimfanya Eddy pia atabasamu. Wote walijikuta wakitabasamu kwa pamoja.

"Mhh, nimesuka kwenye saluni ya hapo nyuma tu." Alijibu akiwa sasa ameanza kuonyesha aibu za kike.

"Najua siku mbili tatu utafumua. Sasa nataka ukifumua uende kwenye saluni hii hii na msusi huyu huyu, akusuke hivi hivi, halafu mimi ndiyo nitalipa, unasikia?"

Ni maneno yaliyomfanya Mwahija aangue kicheko. Ni kicheko cha kujiachia kabisa na akasahau kuwa dakika chache zilizopita alikuwa akimtazama mgeni huyo kwa jicho kali. "Mhhh, yaani utakuja tena huku?"

"Kwa nini nisije? Ukiniambia tu tayari nimeshasuka, basi mimi nakuja huku huku kulipa."

"Haya bwana, nitakwambia."

"Unajua mwanzoni nilikuona mrembo, licha ya kwamba ulininunia, ukawa unanikata jicho kuanzia juu mpaka chini, lakini ulipocheka na kuona mwanya wako, nikagundua kuwa kumbe ni mrembo zaidi kuliko nilivyodhani." Eddy alizidi kumlainisha dada wa watu.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# ANERLISA HATAKI UMBEA WA KIBONGO

MKE wa zamani wa mwanamuziki Ben Pol, Anerlisa ambaye ni raia wa Kenya, amewataka watu kuacha kumfikiria tofauti uhusiano wake na Harmonize.

Akizungumza hivi karibuni, Anerlisa amesema yeye na wasanii wengi wa kiume wa Tanzania wanaelewana kutokana na masuala ya kibiashara na hivyo kuwa karibu na Harmonize ni suala la kawaida.

"Ninaelewana na wasanii wengi wa Tanzania kama Ali Kiba na Harmonize, suala hili siwezi kulijadili sana kwa sababu mimi ni mfanyabiashara na nina watu wengi wanaohitaji kuwa karibu kikazi," amesema.

Hata hivyo, hakutaka kuzungumzia ndoa yake na Ben Pol ambayo ilivunjika baada ya mwanamuziki huyo kubadili dini kuwa Muislam.



# DUNIA YASHTUKA

## RICK ROSS, HAMISA NI MAHABA TUPU

MWANAMITINDO na mwanamuziki kutoka Tanzania, Hamisa Mobetto, amezidi kuitikisa dunia baada ya kila kukicha kufichua mambo mapya kuhusu penzi lake na mwanamuziki maarufu wa Marekani, Rick Ross.

Kuanzia juzi Rick Ross amekuwa akirusha picha akionekana akila bata na Hamisa na kusababisha dunia kushtuka na kuanza kutafuta habari kuhusu mrembo huyo. Katika video za hivi karibuni ameonekana Hamisa akiwa amevaa fulana ya mkali Ross ambayo alivaa juzi huku akikoleza na ujumbe unaosema "Maisha mazuri".

# P' Square warudi rasmi



WAPENZI wa muziki ambao walikosa ladha tamu kutoka kwa ndugu wawili, Peter na paul Okoye, sasa wajiandae kuipata tena, baada ya wasanii hao ambao ni pacha kuamua kuungana tena.

Kipindi cha miaka mitano, wanamuziki hao ambao waliunda kundi la P'Square, walikuwa wametengana kutokana na mgogoro wao wa kifamilia.

Lakini katika taarifa yao ya pamoja, ndugu hao waliotetemesha Afrika, watatumbuiza kwa pamoja katika tamasha lililopewa jina la P'Square reactivated, litakalo fanyika Desemba 18, Mwezi ujao.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAALAND AITAKA REAL
KLABU anayotaka kuhamia mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland iwapo ataondoka Borussia Dortmund mwaka ujao ni Real Madrid, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 bado hajafanya uamuzi kuhusu hali yake ya baadaye. **(Goal)**

### VILLA KUSAJILI BEKI
ASTON Villa wataipa kipaumbele hatua ya kusajili mlinzi wa kati kwenye dirisha la Januari, huku kocha Steven Gerrard akiangalia jinsi ya kumarisha safu hiyo. **(Football Insider)**

### PHILLIPS KUIKATAA MAN
KIUNGO wa kati wa Leeds United na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 25, atakataa uhamisho wa kuhamia katika klabu hasimu ya Manchester United msimu ujao ili kuendelea kubakia pale Elland Road. **(Star)**

### BARCA KUSAJILI MAFOWADI
BARCELONA wanahangaika kwa ajili ya kujuhudi za kuwasaka wachezaji watakaoimarisha safu yao ya ushambuliaji Januari na wanaweza kumsajili mshambulia wa Manchester United mwenye umri wa miaka 28, Jesse Lingard na fowadi wa Uruguay mwenye umri wa miaka 34, Edinson Cavani. **(Mundo Deportivo, via the Sun)**

### MITROVIC HUYO JUVE
MSHAMBULIAJI wa Fulham, Mserbia Aleksandar Mitrovic mwenye umri wa miaka 27, ameandaliwa kwa ajili ya kufanya uhamisho ambao umekuwa ndoto yake kuelekea Juventus. **(Tuttosport, via the Sun)**

### RANGNICK AKARIBIA MAN
MANCHESTER United wanakaribia kabisa kumteua Ralf Rangnick kama kocha wao wa mpito hadi mwishoni mwa msimu huu na raia huyo wa Ujerumani atahusika katika mchakato wa kumchagua mrithi wake hapo Old Trafford. **(Star)**

### TORRES ATAKIWA BARCA
MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 21 analengwa na Barcelona. **(Marca)**

### DEMBELE HUYO NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United inaongoza katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya Ousmane Dembele, huku Manchester United pia wakiwa na nia na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ambaye mkataba wake unaisha kule Barcelona msimu ujao. **(Mundo Deportivo)**

### CONTE KUFANYA TATHMINI
KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, ambaye klabu yake ilifungwa na NS Mura kwenye kombe Ligi ya Europa Conference, amesema anafanya "tathmini" kuhusu wachezaji wake kabla ya kuongea na klabu. **(Mirror)**

### ARTETA KUTOMUUZA PEPE
MIKEL Arteta amekanusha madai kwamba, Arsenal wako tayari kupokea ofa kwa ajili ya winga wao, Coast Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 26 wakati wa dirisha la Januari. **(Metro)**

### BROZOVIC NA MKATABA MPYA
INTER Milan wanamatumaini kwamba, kiungo wake, Marcelo Brozovic mwenye umri wa miaka 29 atasaini mkataba mpya, mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu. **(90 Min)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# 'SANCHO HAKUTAKIWA KUSAJILIWA MAN UNITED'

**Yorke asema uwepo wa Greenwood ulitosha, hakuwa na wakati mzuri na England...**

**MANCHESTER, England**

DWIGHT Yorke amedai Manchester United haikupaswa kumsajili Jadon Sancho kutokana na uwepo wa Mason Greenwood.

Sancho alijiunga kutoka Borussia Dortmund kwa fedha nyingi, lakini ujio wa Cristiano Ronaldo hapo Old Trafford ni kama umemfunika.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alikuwa na kiwango kibovu tangu alipotua hapo na matokeo yake akatemwa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya England kutokana na kutokuwa na muda wa kutosha kucheza pale United.

Hata hivyo, Sancho ambaye amecheza jumla ya dakika 744 kwenye mashindano yote kwa klabu yake hiyo mpya, hatimaye alipata bao kwenye mchezo dhidi ya Villarreal Jumanne baada ya awali kucheza mechi 14 na kupiga mashuti 10 bila kufunga.

Bao hilo alilolifunga kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya lilikuwa la kwanza kwa klabu hiyo, akiwa hajawahi kufunga kabla ya United kuachana na Ole Gunnar Solskjaer na mashetani wekundu hao wapo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi.

Lakini Yorke ameonsha kushangaa kwanini United walimsajili Sancho wakati walikuwa na Greenwood, ambaye alichomoza msimu wa 2019-20 kabla ya kujiwekea rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza chipukizi kufunga katika mechi tatu mfululizo za ufunguzi wa Ligi Kuu England msimu huu.

"Nafikiri watu wanasahau kwamba kuna mchezaji kijana mabaye amekuja na matarajio makubwa," alisema Yorke, ambaye alikuwa mfungaji bora wa United msimu wa 1998-99, akiiambia Stats Perform.

"Hakuwa na wakati mzuri na timu ya England. Tuliona alikosa penalti. Hivyo ni vitu ambavyo wachezaji vijana wanatakiwa kudili navyo.

"Mimi ni shabiki; lakini pengine nafikiri ilikuwa mapema mno kwa sasa kumsajili hapa Man United.

"Nafikiri hatukumuhitaji Sancho katika wakati ambao tulikuwa tayari tuna Greenwood. Nafikiri kwa uhakika kabisa hatukumhitaji kwenye kikosi chetu."







# REAL WAJIPANGA RASMI KWA MBAPPE



**MADRID, Hispania**

MPANGO wa Real Madrid kumsajili nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe umebainishwa, kwa mujibu wa ukurasa wa mbele wa gazeti la Marca la jana Jumamosi.

Nyota huyo wa Ufaransa amekuwa akiwindwa kwa muda mrefu na Real Madrid na sasa wanaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Real Madrid ipo tayari kumsajili nyota huyo wakati wa dirisha la kipindi cha majira ya joto ambapo atakuwa amemaliza mkataba wake na PSG.

Mbappe mwenyewe ameshaweka wazi mara kadhaa namna anavyohusudu kwenda kucheza kule Real Madrid na amekataa kuongeza mkataba mpya na timu hiyo.

Ripoti ya hivi karibuni ilidai kwamba, ofa iliyotolewa na Real Madrid ni "isiyokatalika" na hivyo kuna uwezekano mkubwa Mbappe akatua pale kwenye dimba la Santiago Barnabeu.

Gazeti la Marca pia limeripoti kuwa Madrid wako bize kuhakikisha dirisha dogo la Januari wanaweza kuwachukua kiungo wa Manchester United, Paul Pogba na mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger.

# Mancini aihofia Ureno kufuzu Qatar



**ROME, Italia**

ROBERTO Mancini amekiri Italia isingependa kukutana na Ureno kwenye mchujo wa kufuzu kucheza kombe la Dunia 2022 nchini Qatar kama wakiwatoa North Macedonia.

Mabingwa hao wa Ulaya walipangwa kwenye droo ya Ijumaa kukutana na North Macedonia kwenye nusu fainali Machi mwakani baada ya kushindwa kufuzu moja kwa moja kwenda Qatar.

Italia itacheza dhidi ya Ureno au Uturuki kama wakifanikiwa kuwafunga North Macedonia.

Mabingwa wa Euro 2016, Ureno nao waliingia kwenye mchujo huo baada ya bao la Aleksandar Mitrovic la dakika za majeruhi kuwafanya wapoteze 2-1 dhidi ya Serbia kwenye kundi A.

Kocha wa Italia, Mancini anajiamini timu yake itafuzu, lakini hajaondoa uwezekano wa Cristiano Ronaldo ambaye hizo zinaweza kuwa fainali zake za mwisho za kombe la Dunia, kuwasumbua.

Alisema: "Mara zote tunajiamini na tupo na mtazamo chanya kabisa. Macedonia walikuwa na wakati mzuri kwenye hatua ya kufuzu ya makundi, itakuwa mechi bora zaidi kucheza. Halafu tutaona nini kitatokea kwenye fainali."

Alipoulizwa kuhusu uwezekano wa kukutana na Ureno, alisema: "Tungependa kuwaepuka, na pia hata wao Ureno wasingependa kukutana na Italia."

Katika droo hiyo, Wales wanaweza kukutana na Scotland kama wakiwafunga Austria na Ukraine.

Russia watacheza na Poland, huku mshindi akikutana na Sweden au Jamhuri ya Czech.

## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY

# YANGA YAISHANGAA GEITA KWA FEISAL

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imeonyesha kushangazwa na taarifa za klabu ya Geita Gold kuwataka wachezaji wao Feisal Salum na Mukoko Tonombe kwa staili ya kuulizia bei, badala ya kupeleka ofa rasmi mezani.

Ofisa Habari wa klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli, amesema kwa staili ambayo Geita Gold wanaifanya inaonyesha kuwa hawana uwezo wa kuwanunua wachezaji wao, ila wanachohitaji ni kujua tu bei za wachezaji hao. Hivi karibuni, kumekuwa na barua ikisambaa kwenye mitandao wa kijamii ikionyesha ni ya klabu ya Geita Gold inayoshiriki Ligi Kuu, ambayo ilionyesha kupelekwa kwenye klabu ya Yanga ikiomba kutajiwa bei wa wachezaji Fei Toto na Mukoko kwa ajili ya kutaka kuwasajili kipindi cha dirisha dogo.

Msemaji wa klabu hiyo, Hemed Kivuyo naye alithibitisha kuwa wanawahitaji wachezaji hao na kupeleka barua kwa ajili ya kuuliza bei.

"Mimi nimeona barua hiyo mitandaoni na siyo ofisini, sijui kama imefika ofisini na kama imefika imepolekewa, bado sijaingia masijala, lakini mtu yoyote anaweza kwenda kuulizia bei ya benzi hata kama hana uwezo wa kulinunua, inawezekana nia ni kwenda tu kijiweni na kuanza kuwasimua watu bei ya gari hilo," alisema Bumbuli.

Alisema kuwa walichotakiwa kukifanya Geita Gold ni kuwasilisha ofa mezani ili kufanya majadiliano na si hicho ambacho wamekifanya.

"Kama wanataka kujua bei yao tu sawa, lakini kama wanataka wachezaji waandike barua ya ofa yao na kuiwasilisha ili watu tukae na kujadili, lakini wao wanaulizia bei. Mfano mimi namiliki Vits, nakwenda kuuliza bei ya Prado ambalo sina hata uwezo wa kulinunua. Inawezekana wanauliza bei ili tu kujisifu kuwa tuliuliza bei ya wachezaji Yanga," alisema Bumbuli.



Vijana wa Skauti wakifanya kazi ya kutoa maji yaliotuama katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana, baada ya mvua kunyesha ili uzinduzi wa mashindano ya kuwania kufuzu kucheza Kombe la Dunia kwa walemavu yafanyike. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dodoma yaivaa Coastal Union leo

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu Tanzania bara itaendelea tena leo kwa mchezo mmoja wakati Dodoma jiji watakapokuwa nyumbani kucheza na Coastal Union, katika uwanja wa Jamhuri.

Timu hizo zinashuka dimbani kila moja akihitaji pointi muhimu katika mchezo huo, huku wenyeji wa mechi hiyo Dodoma ikipambana kutumia vema uwanja wake wa nyumbani.

Kikosi cha Dodoma ipo chini ya kocha Mbwana Makata ambapo mechi iliyopita walilazimishwa sare ya 1-1 na Biashara United ya Mara.

Coastal Union kiwa chini ya Mmarekani, Melis Medo iliibuka na ushindi ugenini wa bao 1-0 dhidi ya Polisi Tanzania katika mchezo wa ligi hiyo, uwanja wa Ushirika, Kilimanjaro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Coastal Union, Medo alisema ameandaa kikosi chake na ataingia na mbinu tofauti na mechi iliyopita kuhakikisha wanaendelea kukusanya pointi tatu zingine ugenini.

Alisema baada ya kufanya vizuri kupata matokeo ya pointi tatu dhidi ya Polisi Tanzania, wakarejea uwanjani kufanyia kazi upungufu yao na kuwataka wachezaji kusahau mechi hiyo na kushuka dimbani kutafuta pointi tatu dhidi ya Dodoma jiji FC.

"Nimewaeleza wachezaji wangu kwamba hatuwezi kubaki na matokeo ya mechi iliyopita tumeanza upya na kesho (leo) tunahitaji kupambana kusaka pointi tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi," alisema Medo.

Alisema kuhusu kucheza usiku haitaathiri wachezaji wake licha ya kupata changamoto kidogo kwa sababu ya kutokuwa na uzoefu wa kucheza usiku kulingana na taa za uwanja huo.

Naye kocha wa Dodoma jiji FC, Makata alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo ili kuendelea kubaki katika nafasi katika msimamo wa ligi.


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA



PAKUA SASA

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 28 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2382 | Gaziantep BB vs Konyaspor | 2.68 | 3.18 | 2.58 |
| 14:15 | 2409 | Sparta Rotterdam vs Ajax | 15.71 | 7.66 | 1.13 |
| 14:30 | 2983 | Udinese vs Genoa | 1.77 | 3.65 | 4.51 |
| 15:00 | 1901 | Livingston vs Rangers | 8.72 | 4.96 | 1.32 |
| 15:00 | 1903 | FC Ingulets vs Shakhtar Donetsk | 16.44 | 7.15 | 1.11 |
| 15:00 | 5989 | St Etienne vs Paris St Germain | 7.14 | 5.12 | 1.37 |
| 15:30 | 2418 | Sheffield Utd vs Bristol City | 1.51 | 4.02 | 5.89 |
| 16:00 | 3719 | Olympiakos vs Volos | 1.18 | 6.32 | 13.82 |
| 16:00 | 5057 | Odense vs Nordsjalland | 1.89 | 3.79 | 3.54 |
| 16:00 | 5790 | Betis vs Levante | 1.66 | 4.00 | 4.80 |
| 16:00 | 5861 | Leganes vs Las Palmas UD | 2.19 | 3.00 | 3.44 |
| 16:15 | 3351 | FC Zurich vs BSC Young Boys | 3.10 | 3.65 | 2.09 |
| 16:30 | 2904 | Utrecht vs Heracles Almelo | 1.61 | 4.03 | 4.72 |
| 16:30 | 3357 | Rubin Kazan vs Dinamo Moscow | 3.39 | 3.39 | 2.04 |
| 16:30 | 4952 | Twente vs Feyenoord | 4.02 | 3.78 | 1.77 |
| 17:00 | 1130 | Bordeaux vs Brest | 2.37 | 3.38 | 2.88 |
| 17:00 | 1799 | Manchester City vs West Ham | 1.33 | 5.31 | 8.42 |
| 17:00 | 2072 | Brentford vs Everton | 2.22 | 3.20 | 3.35 |
| 17:00 | 2786 | Lorient vs Rennes | 4.37 | 3.83 | 1.74 |
| 17:00 | 3375 | Spezia vs Bologna | 2.99 | 3.44 | 2.30 |
| 17:00 | 3425 | AC Milan vs Sassuolo | 1.56 | 4.40 | 5.20 |
| 17:00 | 3618 | IFK Goteborg vs Ostersunds | 1.20 | 5.77 | 10.58 |
| 17:00 | 3691 | Reims vs Clermont Foot | 2.41 | 3.13 | 3.03 |
| 17:00 | 5104 | Monaco vs Strasbourg | 1.66 | 3.93 | 4.78 |
| 17:00 | 5502 | Leicester vs Watford | 1.62 | 4.20 | 4.90 |
| 17:00 | 5594 | Burnley vs Tottenham | 3.56 | 3.51 | 2.02 |
| 17:30 | 2324 | Eintracht Frankfurt vs Union Berlin | 2.32 | 3.40 | 2.95 |
| 18:00 | 1157 | Brondby vs Randers | 2.06 | 3.50 | 3.30 |
| 18:00 | 3267 | Celtic vs Aberdeen | 1.28 | 5.32 | 9.45 |
| 18:15 | 1685 | Espanyol vs Real Sociedad | 3.20 | 3.25 | 2.28 |
| 18:30 | 2346 | Maritimo vs Pacos Ferreira | 2.66 | 3.10 | 2.66 |
| 18:30 | 4427 | FC Luzern vs FC Basel | 2.71 | 3.50 | 2.38 |
| 18:45 | 3790 | Heerenveen vs PSV Eindhoven | 5.33 | 4.44 | 1.50 |
| 19:00 | 3213 | Rosenborg vs Bodo Glimt | 2.61 | 3.59 | 2.42 |
| 19:00 | 3298 | Josko Ried vs Rapid Vienna | 4.25 | 3.67 | 1.69 |
| 19:00 | 4095 | Montpellier vs Lyon | 4.07 | 4.17 | 1.73 |
| 19:00 | 4137 | Yeni Malatyaspor vs Galatasaray | 4.24 | 3.75 | 1.75 |
| 19:30 | 1493 | Kalmar vs Malmo | 4.34 | 3.57 | 1.70 |
| 19:30 | 2956 | RB Leipzig vs Bayer Leverkusen | 1.81 | 3.99 | 3.84 |
| 19:30 | 5698 | Chelsea vs Manchester Utd | 1.58 | 4.11 | 5.41 |
| 20:00 | 1247 | Aalborg vs Copenhagen | 2.90 | 3.34 | 2.32 |
| 20:00 | 3760 | Sparta Prague vs Slovan Liberec | 1.38 | 4.90 | 7.60 |
| 20:00 | 5269 | CSKA Moscow vs Zenit St Petersburg | 3.83 | 3.58 | 1.85 |
| 20:00 | 5996 | Roma vs Torino | 1.70 | 3.91 | 4.61 |
| 20:30 | 3090 | Cadiz CF vs Atletico Madrid | 6.82 | 4.01 | 1.51 |
| 20:30 | 5642 | Panathinaikos vs Panetolikos | 1.42 | 4.23 | 7.48 |
| 21:00 | 2344 | Sporting Lisbon vs Tondela | 1.18 | 6.32 | 13.82 |
| 22:45 | 2837 | Napoli vs Lazio | 1.79 | 3.88 | 4.08 |
| 22:45 | 3266 | Marseille vs Troyes | 1.53 | 4.30 | 5.60 |
| 23:00 | 5903 | Real Madrid vs Sevilla FC | 1.75 | 3.72 | 4.57 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Novemba 28, 2021
Nipashe




## 'Sancho hakutakiwa kusajiliwa Man United'

HABARI UK 21

## Yanga hesabu kamili kwa Mbeya kwanza

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga kinaondoka leo kuelekea Mbeya tayari kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya Kwanza utakaopigwa katika uwanja wa Sokoine.

Yanga itaondoka na wachezaji 22, kuelekea mkoani humo huku wakiendelea kukosa huduma ya nyota wake wawili Abdallah Shaibu 'Ninjas na Yacouba Songne ambao ni majeruhi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, alisema baada ya kutoka Lindi dhidi ya Namungo FC na sasa mahesabu ni kuhakikisha wanapata ushindi dhidi ya Mbeya Kwanza.

Alisema ameona changamoto ya uwanja mbovu wa Ilulu na kupoteza pointi mbili hali ambayo hatakiwa ijirudie katika mchezo dhidi ya Mbeya Kwanza na kuwasuka viungo wake kwa ajili ya kutengeneza nafasi nyingi.

Alisema washambuliaji wake wamekuwa na mazoezi magumu ya kumalizia nafasi kitu ambacho alikigundua katika mchezo uliopita dhidi ya Namungo ambao ulimalizika kwa sare ya 1-1.

"Uwanja ulitupa shida ni lazima tujiandae pia kwa mazingira ya kukutana na viwanja vya namna hiyo, uwanja ulitupa wakati mgumu, lakini hata sisi yapo mambo ambayo hatukufanya vizuri na kutakiwa kujiandaa kwa ajili ya mechi ijayo," alisema.

Alisema wamekuwa na mazoezi ya kuangalia upya akili ya wachezaji wake na kutafuta nafasi kuanzia eneo la kiungo na washambuliaji ili kuhakikisha wanatengeneza nafasi zaidi ya kupata ushindi katika viwanja vya aina ya Ilulu na Sokoine anapokwenda kucheza.

"Mchezo wetu dhidi ya Mbeya Kwanza hautakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wetu hawajawahi kupata nyumbani, utakuwa ni fainali nyingine kabla ya kucheza na Simba Desemba 11, mwaka huu," alisema

9 770856 541002 >



Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa (kushoto), akiikagua timu ya Taifa ya Walemavu ya Tanzania, wakati wa mashindano ya timu za walemavu za Afrika kuwania kufudhu kucheza michuano ya Kombe la Dunia jijini Dar es Salaam jana yanayotarajia kufanyika mwakani nchini Uturuk. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NI SIMBA VS RED ARROWS

## ●●●Kocha Franco atamba morali ya wachezaji iko juu, ushindi ni lazima leo ...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania, Simba, leo watakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuipeperusha bendera ya nchi, watakapoivaa Red Arrows ya Zambia kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya mtoano, Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Simba inacheza kombe hilo, baada ya kuondolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy kwa tofauti ya goli la ugenini, baada ya kufungana jumla ya mabao 3-3 kwenye mechi za nyumbani na ugenini zilizochezwa Oktoba, mwaka huu.

Itakuwa ni mara ya kwanza kwa Simba kucheza Kombe la Shirikisho tangu mwaka 2018. Mara ya mwisho Simba kucheza kombe hilo ilikuwa ni Machi 17,mwaka 2018, ilipotoka suluhu na Al Masry ya Misri, mechi iliyochezwa nchini Cairo.

Ilikuwa ni mechi ya mkondo wa pili kwani mechi iliyofanyika Dar es Salaam Machi 7, mwaka huo huo, timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. Simba ilitolewa kwenye michuano hiyo kwa faida ya bao la ugenini kwa Al Masry, na Wamisri hao wakatinga kwenye hatua ya makundi ya kombe hilo.

Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema kuwa itakuwa ni mechi yake ya kwanza ya kimataifa na ya kwanza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini kutokana na mazoezi ambayo wameyafanya na morali anayoiona kwa vijana wake, anaamini kuwa wanakwenda kushinda mechi hiyo ili kujijengea mazingira mazuri kwenye mechi ya marudiano nchini Zambia Desemba 5, mwaka huu.

"Ikumbukwe kuwa hii si mechi ya dakika 90, ni mechi ya nyumbani na ugenini, hivyo kuna mikakati tumeweka kwa ajili ya kufanikisha kupita hapa kwenye hatua ya mtoano. Tuna kikosi kizuri na mashabiki watarajie kuona mabadiliko ya wachezaji na mfumo kwenye kila mechi tunayocheza," alisema kocha huyo.

Nahodha wa timu hiyo, John Bocco, amesema wapo timamu kimwili na kiakili kuelekea mechi hiyo na watorudia tena makosa waliyoyafanya kwenye mechi dhidi ya Jwaneng Galaxy.

"Kimwili kiakili tupo timamu, tumefanya mazoezi ya kutosha na tuna morali pia. Mchezo hautokuwa rahisi kwa sababu tunahitaji matokeo nyumbani ili tujiwekee mazingira mazuri kunapokwenda ugenini," alisema Bocco.

"Najua tumesomana, wao wametusoma na sisi tumewasoma, lakini sisi tumerekebisha makosa yote yaliyotokea kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa. Tunachukulia tuliteleza na hatutorudia tena makosa, ila tunawataka wanachama na mashabiki wote wajitokeze kwa wingi kama ambayo huwa wanafanya tunapocheza," aliongeza Bocco.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez, alisema kuwa wanakwenda kucheza mechi ngumu kwa sababu karibuni timu zote zinazocheza na Simba hucheza kwa kupania kwa sababu wanataka waonekane na kusajiliwa, huku akiongeza kuwa lengo la klabu hiyo ni kufika nusu fainali.

"Tunataka kuiwakilisha nchi vizuri kama ambavyo tumekuwa tukifanya. Tunataka kuibeba nchi mabegani kulinda nafasi nne," alisema Barbara.

Aliongeza; "Safari hii tumeziba njia zote ambazo zilitufanya tuteleze kwenye mechi zilizopita na tumechukua hatua mbalimbali kwa kile kilichotokea kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa. Najua mechi itakuwa ngumu, lakini huo iko hivyo, mechi zote za timu yetu zinakuwa ngumu kwa sababu wachezaji wa timu pinzani wanataka njia ya kuingilia Simba. Safari hii tunataka kufika nusu fainali kwenye kombe hili."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9